Kiswahili

Kiongozi cha Mwalimu

Darasa la Saba


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

Cheti cha Ithibati

Na. 384

Jina la Chapisho: Kiswahili Kiongozi cha Mwalimu Darasa la Saba

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978 - 9987 - 09 - 155 - 3

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 08 Julai 2020 kuwa Kiongozi cha Mwalimu kwa ajili ya Darasa la Saba katika ngazi ya elimu ya Msingi nchini Tanzania kulingana na Kitabu cha Mwanafunzi cha Kiswahili Darasa la Saba, Mwaka 2020

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

Taasisi ya Elimu Tanzania

KIONGOZI_KISW.indd 1 7/23/21 3:23 PM

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2020

Toleo la Kwanza 2020
Chapa ya Pili 2021

ISBN: 978-9987-09-155-3

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
Dar es Salaam - Tanzania

Simu: +255 735 041 170 /+255 735 041 168
Barua pepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kukitoa kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

KIONGOZI_KISW.indd 2 7/23/21 3:23 PM

Yaliyomo

Ukurasa

Shukurani ..... **v**

Utangulizi ..... **vi**

Sura ya Kwanza

Mashairi **1**

Sura ya Pili

Utenzi **16**

Sura ya Tatu

Ngonjera **23**

Sura ya Nne

Vitendawili **30**

Sura ya Tano

Tutumie methali zetu **38**

Sura ya Sita

Matumizi ya nahau **47**

Sura ya Saba

Aina za maneno **55**

Sura ya Nane

Hadithi **63**

Sura ya Tisa

Risala **69**

Sura ya Kumi

Kusoma magazeti **78**

KIONGOZI_KISW.indd 3 7/23/21 3:23 PM

Sura ya Kumi na Moja
Barua ya kirafiki na rasmi **86**

Sura ya Kumi na Mbili
Kadi za mialiko **95**

Sura ya Kumi na Tatu
Insha **102**

Sura ya Kumi na Nne
Hotuba **110**

Sura ya Kumi na Tano
Ufupisho **117**

Sura ya Kumi na Sita
Uwasilishaji wa hoja **125**

KIONGOZI_KISW.indd 4 7/23/21 3:23 PM

Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki waliofanikisha uandishi wa kiongozi hiki cha mwalimu.

TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wafuatao:

Waandishi: Mwl. Rose S. Chipindula, Mwl. Melina A. Yohana, Mwl. Samwel M. Magutu, Mwl. Tumaini M. Mahendeka, Mwl. Adelgot J. B. Mapunda, Mwl. Aurelia F. Mutajunwa, Mwl. Jivitius C. Sabatho na Mwl. Monica W. Manyanga

Wahariri: Prof. David P. B. Massamba, Prof. Kulikoyela K. Kahigi, Dkt. Rehema O. Stephano, Dkt. Adventina A. Buberwa, Mwl. Titus Mpemba, Mwl. Saul S. Bichwa (Maudhui) na Bi. Gertrude Joseph (Lugha - BAKITA)

Msanifu: Bw. Silvanus A. Mihambo

Wachoraji: Bw. Fikiri A. Msimbe na Alama Art and Media Production Limited

Mratibu: Mwl. Rose S. Chipindula

Pia, TET inatoa shukurani kwa walimu wote walioshiriki katika ujaribishaji wa kiongozi hiki cha mwalimu. Vilevile, TET inatoa shukurani za pekee kwa shirika la "Global Partnership for Education (GPE)" kupitia mradi wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) uitwao "Literacy and Numeracy Education Support (LANES II)" kwa ufadhili wao uliofanikisha kazi ya uandishi na uchapaji wa kiongozi hiki.

Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kusimamia kwa karibu zoezi zima la uandishi na uchapaji wa kiongozi hiki.

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
Taasisi ya Elimu Tanzania

KIONGOZI_KISW.indd 5 7/23/21 3:23 PM

Utangulizi

Kiongozi hiki ni cha tano katika mfululizo wa viongozi vitano vya somo la Kiswahili kuanzia Darasa la Tatu hadi la Saba, kilichoandaliwa mahususi kwako mwalimu wa Darasa la Saba. Kiongozi hiki kimeandaliwa kulingana na muhtasari wa somo la Kiswahili wa mwaka 2019 uliotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Lengo kuu la kiongozi hiki ni kukupa mwalimu mbinu na maarifa ya kufundisha somo la Kiswahili katika Darasa la Saba. Katika kiwango hiki, mwanafunzi anatakiwa aweze kumudu vizuri stadi za kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika Kiswahili katika miktadha mbalimbali.

Lugha iliyotumika katika matini, msamiati, miundo, mazoezi ya lugha, methali, nahau na vitendawili ni ya kiwango cha juu kuliko ya Darasa la Sita. Mbinu mbalimbali za ufundishaji zimependekezwa. Una uhuru wa kubuni mbinu nyingine kulingana na mazingira, hali ya mahali, idadi na uwezo wa wanafunzi wako ili kuleta ufanisi katika ujifunzaji. Katika mchakato wote wa ufundishaji na ujifunzaji, washirikishe wanafunzi katika mazungumzo, kuimba, kuchora, kuigiza, kutamba na kughani.

Vipengele vya ufundishaji wa stadi za lugha

Vifuatavyo ni vipengele muhimu ambavyo vitakusaidia kufundisha stadi za lugha katika Darasa la Saba.

1. Msamiati

Ni jambo muhimu kuhakikisha kuwa wanafunzi wanafahamu maneno yote mapya na kuyatumia katika sentensi. Msamiati ufundishwe kwa kutumia vitu halisi, picha na vielelezo, maelezo, vitendo, maigizo na maonesho. Kwa hiyo, huna budi kutayarisha zana za kutosha za kufundishia na kujifunzia, hasa zinazopatikana katika mazingira yako. Vidokezo vifuatavyo ni muhimu:

KIONGOZI_KISW.indd 6 7/23/21 3:23 PM

(a) Kutumia vitu halisi
Ni muhimu utumie vitu halisi katika kufundisha msamiati kwa kuwa, wanafunzi wanapoona, huelewa kwa urahisi.

(b) Kutumia picha na vielelezo mbalimbali
Iwapo utashindwa kupata vitu halisi, tumia picha na vielelezo. Picha na vielelezo vitayarishwe mapema na viwe vikubwa vya kutosha ili viweze kuonekana kwa urahisi kwa wanafunzi wote. Viwe na mvuto na uhalisia ili kueleza dhana kwa usahihi. Zingatia wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Kwa mfano, tumia picha na vielelezomguso ili kuwasaidia wanafunzi wasioona au wenye uoni hafifu.

(c) Kutumia vitendo
Inafaa maneno mengine hasa vitenzi na vivumishi yafundishwe kwa vitendo. Kwa mfano, chagua mwanafunzi na kumpa kifutio na kumwelekeza aende kufuta ubao. Mwanafunzi atafanya kama alivyoelekezwa. Uliza swali. _____ (*Taja jina la mwanafunzi*) alikuwa anafanya nini? Pokea majibu; kisha, eleza kuwa ulikuwa unafundisha neno "futa".

2. Miundo

Muundo ni mpangilio wa maneno na uhusiano wake katika sentensi. Katika muundo mmoja, inawezekana kutunga sentensi kadhaa zenye maana tofauti.

Katika Kitabu cha Mwanafunzi, alama za kistari (yaani ____) na dotidoti (yaani……..) zinatumika kuonesha nafasi ya kujaza miundo iliyolengwa. Alama ya kistari huonesha kuwa neno halijakamilika. Alama ya dotidoti huonesha kuwa neno au maneno hayapo. Katika miundo, nafasi hizo zinatakiwa zijazwe. Nafasi ya kistari itajazwa na sehemu ya neno na dotidoti itajazwa kwa neno au maneno. Waongoze wanafunzi kujaza nafasi hizo. Kwa mfano:

KIONGOZI_KISW.indd 7 7/23/21 3:23 PM

(a) Muundo "ana____" unaweza kujazwa na kuwa: analima, anasoma, anaimba, anatembea na kuendelea.

(b) Muundo ".....ata__" unaweza kujazwa ukawa Bibi atakuja.

Miundo ifundishwe kwa lugha rahisi na inayoeleweka. Irudiwerudiwe ili wanafunzi waizoee na kujenga kumbukumbu. Sentensi zinazotungwa kusisitiza miundo lazima zilingane na mazingira na maisha ya wanafunzi ili waweze kuzitumia katika maisha yao ya kila siku. Andaa mazoezi ya ziada kutokana na misingi ya sura inayofundishwa.

3. Methali

Methali zifundishwe kadiri zinavyotokea katika hadithi au zijengewe maelezo yanayohusiana na mazingira zinamotumika. Eleza methali kwa kutumia masimulizi yanayohusiana na maisha ya kila siku. Ili wanafunzi wagundue maana za methali hizo, unaweza kufundisha methali zinazofanana au zilizo kinyume na zile zilizomo katika hadithi. Ufundishaji wa methali bila kuzihusisha na mazingira ya maisha haufai. Wanafunzi waelekezwe kutoa mianzo au miisho ya methali zao na wengine wamalizie. Pia, wanafunzi waongozwe kutumia methali katika miktadha mbalimbali.

4. Vitendawili

Fundisha vitendawili kwa kuwapa wanafunzi nafasi ya kutega na kutegua vitendawili vyao. Waelekeze kupeana mji kila wanaposhindwa kupata jibu sahihi. Uhusiano uliopo kati ya kitendawili na jibu lake ujadiliwe. Vitendawili pia vinaweza kutumiwa kama chemshabongo mwanzo wa somo la Kiswahili. Vitendawili vipya vyenye mantiki vikubaliwe. Kumbuka kwamba vitendawili hutofautiana kulingana na mazingira.

5. Misemo na nahau

Fundisha misemo na nahau kwa maelezo, picha, matendo, vitu halisi na majadiliano. Waongoze wanafunzi jinsi ya kutumia

KIONGOZI_KISW.indd 8 7/23/21 3:23 PM

misemo na nahau hizo katika sentensi. Kwa mfano, maneno yako yalimkata maini (Maneno yako yalimuudhi kupindukia).

6. Ufahamu

Lengo la kusoma ni kuelewa kilichoandikwa, yaani ufahamu. Kuna njia mbalimbali za kufundishia kusoma. Unashauriwa kufuata mwongozo uliotolewa katika kitabu hiki. Hata hivyo, uwe tayari kubadili njia iwapo utapata vikwazo, kwani ufanisi wa mwanafunzi ndio lengo letu. Zifuatazo ni njia mbalimbali za kusoma:

(a) Kusoma kimya

Katika somo la kusoma kimya, waelekeze wanafunzi kusoma kimya bila kufungua mdomo. Wanafunzi wasome sura yote na kujibu maswali ya ufahamu. Licha ya maswali yaliyomo kitabuni, tunga maswali mengine ya nyongeza kuhusiana na sura inayohusika.

(b) Kusoma kwa sauti

Lengo la kusoma kwa sauti ni kuwawezesha wanafunzi kusoma kwa lafudhi sahihi ya Kiswahili kwa kuzingatia sauti ya kutosha, matamshi, shadda, kiimbo, matumizi ya alama za uandishi kwa usahihi na hisia. Katika somo la kusoma kwa sauti, onesha mfano wa usomaji mzuri. Pia, teua wanafunzi wengi kadiri inavyowezekana kusoma kwa sauti. Hii itategemea muda, idadi ya wanafunzi na kiwango chao cha usomaji.

(c) Kusoma kwa ziada

Lengo la kusoma kwa ziada ni kumwezesha mwanafunzi kusoma kwa ufahamu na kwa kasi stahiki na kumwongezea maarifa. Kusoma kwa ziada pia humjengea mwanafunzi tabia ya kupenda kujisomea. Ongoza usomaji huu. Yafuatayo yazingatiwe kutekeleza jambo hili:

(i) Waelekeze sura ya kusoma katika kipindi hicho.

(ii) Wanafunzi wasome kimya.

(iii) Waulize maswali. Wanafunzi wajibu maswali hayo

KIONGOZI_KISW.indd 9 7/23/21 3:23 PM

kwa kuzungumza au kwa kuandika. Waongoze wanafunzi kutoa muhtasari wa habari waliyosoma.

(iv) Katika baadhi ya vipindi, badala ya kujibu maswali, wanafunzi waelekezwe kuchora, kusimulia, kuigiza au kuimba ili kusisitiza maarifa waliyoyapata.

(v) Inafaa somo la kusoma kwa ziada lifanyike mara moja ndani ya wiki mbili.

7. Mazoezi ya lugha

Katika kitabu hiki, kuna mazoezi mbalimbali ya lugha kwa kila sura. Mazoezi hayo yamejumuisha uchaguzi wa jibu sahihi, kujaza nafasi, kueleza maana za maneno, kuunganisha sehemu mbili za sentensi, umoja na wingi, kubadili nyakati na mengineyo. Fundisha zoezi moja au mawili ya lugha kwa kipindi kimoja na kuongeza mazoezi kulingana na mazingira na uwezo wa wanafunzi. Hakikisha wanafunzi wanaandika kwenye madaftari yao mazoezi yote wanayopaswa kuandika.

8. Utungaji

Sehemu kubwa ya mazoezi ya utungaji katika darasa hili ni ya kuongozwa. Uongozi huo umefanywa kwa:

(a) Kuchagua na kupanga sentensi zilizochanganyika, hasa zilizotokana na habari iliyosomwa au kuzungumzwa.

(b) Kutumia picha. Wanafunzi wanaweza kuchora, kama wataelekezwa na mwalimu kufanya hivyo. Wanaweza pia kuchorewa picha zinazohusu habari fulani. Wanafunzi wanatakiwa kutoa maelezo kuhusu picha moja au zaidi zilizotolewa.

(c) Kukamilisha habari.

(d) Kusimulia na kuelezea hadithi au habari mbalimbali. Wanafunzi wahimizwe kuigiza, kuimba, kutenda na kuitikia.

(e) Kuuliza maswali ambayo majibu yake yataunda hadithi.

Toa uzito sawa wa mazoezi ya utungaji wa mdomo na wa kuandika. Hii itawasaidia wanafunzi kukuza uwezo wa kujieleza kwa mdomo na kwa maandishi.

KIONGOZI_KISW.indd 10 7/23/21 3:23 PM

9. Ushairi

Ushairi ni uwanja mwingine wa fasihi. Katika kiwango hiki, mwanafunzi asome na kuimba mashairi, tenzi na ngonjera. Pia, atambue vina, mizani, mishororo na urari katika mashairi. Vilevile, aelewe mawazo makuu na ujumbe uliomo katika shairi.

10. Mwandiko

Kazi ya kufundisha mwandiko iliyoanza Darasa la Kwanza iendelezwe na kuimarishwa katika darasa hili. Sisitiza uumbaji mzuri wa herufi, hati ya kuunga, ukataji wa maneno kwa kuzingatia silabi na nafasi kati ya neno na neno. Pia, alama za uandishi zisisitizwe. Sisitiza usahihi wa mwandiko katika kila somo linalohusisha kuandika.

11. Imla

Ni somo ambalo hupima uwezo wa wanafunzi wa kusikiliza na kuandika kwa usahihi kile walichosomewa na mwalimu. Wanafunzi wengi hawawezi kuandika habari vizuri kwa kufuata taratibu na alama za uandishi. Vilevile, hawawezi kuandika kwa kasi kwa kufuata msomaji anavyosoma. Fundisha uandishi wa imla kwa kuzingatia kanuni.

12. Matayarisho/maandalizi ya somo

Soma Kitabu cha Mwanafunzi na Kiongozi cha Mwalimu kwa makini na uelewa kabla ya kufundisha. Hii itakusaidia kuelewa kwa undani vipengele vyote unavyotakiwa kufundisha. Hakikisha unaandaa somo lako vizuri kama inavyotakiwa.

13. Fikiri

Waongoze wanafunzi kujibu swali katika kipengele cha fikiri katika kila sura kabla ya kusoma. Swali hilo litakusaidia kupata maarifa ya awali aliyonayo mwanafunzi kuhusu sura inayohusika.

KIONGOZI_KISW.indd 11 7/23/21 3:23 PM

14. Mgawanyo wa vipindi

Katika mwaka wa masomo, kutakuwa na siku 194 ambazo ni sawa na wiki 39 za masomo. Makadirio ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 40. Katika darasa hili, kuna vipindi 7 vya Kiswahili kwa wiki. Hata hivyo, mapendekezo haya yanaweza kubadilika kulingana na mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

15. Mrejesho kwa wanafunzi

Sahihisha kazi zote za wanafunzi na kuwapa mrejesho. Ni vema kufanya masahihisho darasani ili kila mwanafunzi atambue kosa lake na kujisahihisha.

KIONGOZI_KISW.indd 12 7/23/21 3:23 PM

Sura ya Kwanza

Mashairi

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza zaidi sifa za mashairi ya kimapokeo na ya kisasa. Atachambua na kueleza maudhui yaliyomo katika mashairi. Vilevile, atatunga mashairi ya kimapokeo na ya kisasa ili kujijengea umahiri wa kutunga mashairi.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kueleza sifa za mashairi ya kimapokeo
(b) kueleza sifa za mashairi ya kisasa
(c) kusoma na kughani shairi
(d) kuchambua maudhui yaliyomo kwenye mashairi
(e) kutunga mashairi ya kimapokeo na ya kisasa
(f) kueleza taswira katika shairi

Mahitaji: shairi la mfano, matini mbalimbali zenye mashairi, manila na kalamu rashasha

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujadili mambo ya kuzingatia katika utunzi wa mashairi kwa mujibu wa kipengele cha *fikiri* ukurasa wa kwanza katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya shairi la kimapokeo lililopo ukurasa wa kwanza hadi wa nne katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(c) Waulize wanafunzi maswali yafuatayo:
    (i) Shairi hili linahusu nini?
    (ii) Kila ubeti wa shairi ulilosoma una mishororo mingapi?
(d) Waongoze wanafunzi kujadili kuhusu lugha ya picha (taswira) iliyotumika katika shairi hilo.
(e) Waongoze wanafunzi kughani shairi walilolisoma kwa mahadhi tofautitofauti.

KIONGOZI_KISW.indd 1 7/23/21 3:23 PM

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kusoma na kughani shairi la kimapokeo lililopo ukurasa wa kwanza hadi wa nne katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(b) Waongoze wanafunzi kubaini msamiati kutokana na shairi. Andika ubaoni msamiati huo.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia msamiati uliopo ubaoni. Toa maelezo mafupi kuhusu usomaji wa shairi kwa kuzingatia kiimbo na hisia.

(d) Wakumbushe wanafunzi kuhusu dhana ya 'vina', 'mizani' na 'mishororo.'

(e) Toa maelezo kuhusu mashairi ya kimapokeo.

(f) Waongoze wanafunzi kusoma mmojammoja kwa zamu, kwa kuzingatia jinsi. Hakikisha wengi wanapata nafasi ya kusoma.

(g) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza katika usomaji na kuzisahihisha. Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo. Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

(h) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **4** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Andika maneno yafuatayo ubaoni: *azimu, kabwa, chemchemi, mlizamu, kiini, beza, muhali, pote, janibu* na *jikusuru*. (neno chemchemi kwenye shairi linasomeka kama chemchemu kutokana na utafutaji wa vina, neno halisi ni chemchemi)

(b) Waongoze wanafunzi kusoma maneno hayo kwa sauti.

(c) Waongoze wanafunzi kueleza maana za maneno hayo.

(d) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kila neno lililopo ubaoni.

Mfano: *Juma ana **kipaji** cha uchoraji na ufinyanzi.*

(e) Waongoze wanafunzi kubaini makosa na kuyarekebisha.

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **4** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(g) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia usahihi wa sentensi.

KIONGOZI_KISW.indd 2 7/23/21 3:23 PM

Somo la 4: Imla

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo hili. Sisitiza wanafunzi waandike imla hiyo kwa hati ya wima na ya kuunga. Pia, wazingatie alama za uandishi.

(b) Wasomee wanafunzi habari ifuatayo kwa kasi ya kawaida. Wanafunzi wasikilize bila kuandika.

Juma alihitimu Darasa la Saba katika Shule ya Msingi Mapinduzi. Licha ya masomo ya darasani, alikuwa na kipaji cha kuogelea. Alitumia kipaji chake kuokoa watu waliozama majini. Siku moja alimwokoa mzee. Mzee yule alifurahi sana na kuahidi kumpeleka kwenye chuo cha uogeleaji. Juma alienda nyumbani kuwaaga wazazi tayari kwa kwenda chuoni. Juma alisoma kozi ya uogeleaji kwa bidii. Alihitimu mafunzo yake na sasa ni mwogeleaji wa kimataifa.

(c) Wasomee tena kwa mara ya pili kwa kufuata vituo na alama za uandishi huku wakiandika kwenye madaftari yao.

(d) Wasomee taratibu huku wao wakifuatisha na kuhakiki kile walichokiandika.

(e) Kusanya madaftari papo hapo na sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia uumbaji wa herufi, usafi wa kazi, nafasi kati ya neno na neno, matumizi ya alama za uandishi, matumizi ya herufi kubwa na hati ya wima na ya kuunga.

Somo la 5: Miundo

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu miundo.

(b) Nakili ubaoni miundo yote iliyopo katika zoezi la 3 ukurasa wa **5** katika Kitabu cha Mwanafunzi. **Mfano:** …… lakini …… ……la ….., ……. za ……

(c) Waongoze wanafunzi kusoma kwa sauti miundo hiyo.

(d) Waongoze wanafunzi kujadili kuhusu kanuni za miundo hiyo.

(e) Toa mifano ya sentensi zenye miundo iliyopo katika zoezi la 3 ukurasa wa **5** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(f) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

KIONGOZI_KISW.indd 3 7/23/21 3:23 PM

(g) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa **5** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Sentensi hizo zisiwe zile zilizotolewa kwenye mifano ya darasani.
(h) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuangalia usahihi katika matumizi ya miundo kwenye sentensi na alama za uandishi.

Somo la 6: Methali

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo la methali.
(b) Waongoze wanafunzi kutaja methali mbalimbali.
(c) Andika ubaoni methali hizo.
(d) Andika baadhi ya mianzo au miisho ya methali; kisha, waongoze wanafunzi kukamilisha methali hizo.
(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa **5** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

1. *Jina jema*
2. *halichukuliwi shoka*
3. *usilitukane*
4. *ni mtoto kucheka*
5. *ni mateke*
6. *Amnyimaye punda adesi*
7. *kuliko mwongo*
8. *kama hukijui ulacho*
9. *ni nyumba ya njaa*
10. *usikatae wito*

Somo la 7: Mazoezi ya lugha

A. Kupigia mstari vihusishi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu dhana ya vihusishi kwa kifupi. Kumbuka vihusishi (H) ni maneno yanayohusisha maneno mengine katika tungo.
(ii) Waongoze wanafunzi kutaja vihusishi mbalimbali.

KIONGOZI_KISW.indd 4 7/23/21 3:23 PM

(iii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi zenye vihusishi ndani yake.
(iv) Waongoze wanafunzi kubaini vihusishi katika sentensi zilizotungwa.
(v) Tumia mifano iliyopo kwenye zoezi la 5 A kuwaongoza wanafunzi kufanya zoezi hilo lililopo ukurasa wa **5 - 6** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Mpera umeota katikati ya mipapai.
(ii) Mtoto ameokota ganda la muwa.
(iii) Mimi ninapenda dagaa wa kukaanga.
(iv) Nyumba yetu imejengwa kando ya bahari.
(v) Mama anapasua mbao za kuuza.
(vi) Kiti nilichokalia jana ni cha mtoto.
(vii) Nyafuru amesimama ukingoni mwa barabara.
(viii) Makoba amebeba viti vya mjomba.
(ix) Mbwa wetu anakunywa maji kwa kulapa.
(x) Kulwa ameokota embe chini ya mwembe.

B. Kuandika umoja au wingi wa maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo la umoja na wingi.
(ii) Andika maneno kadhaa ubaoni, kisha waongoze wanafunzi kuyabadili katika wingi.
(iii) Tumia mifano iliyopo zoezi la 5 B lililopo ukurasa wa **6** kwenye Kitabu cha Mwanafunzi kuongoza mjadala kuhusu kubadili maneno katika umoja au wingi.
(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 B lililopo ukurasa wa **6** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) vyura
(ii) kigoda
(iii) watu
(iv) simba
(v) nyoka
(vi) soda
(vii) makopo
(viii) mlima
(ix) vyuma
(x) jengo

KIONGOZI_KISW.indd 5 7/23/21 3:23 PM

C. Kubadili sentensi kuwa katika wakati uliopo hali ya kuendelea
Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo la wakati uliopo hali ya kuendelea.
(ii) Andika sentensi za nyakati tofautitofauti ubaoni.
(iii) Waongoze wanafunzi kuzibadili kuwa katika wakati uliopo hali ya kuendelea.
(iv) Andika sentensi hizo ubaoni.
(v) Waongoze wanafunzi kubaini makosa yaliyojitokeza katika sentensi hizo na kuyarekebisha.
(vi) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 C lililopo ukurasa wa **6** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

*(i) Juma a**na**jifunza kutunga shairi.*
*(ii) Mwanakwao a**na**kula chakula chote.*
*(iii) Shangazi a**na**enda kumwandikisha mdogo wangu shuleni.*
*(iv) Kikundi chetu ki**na**fuga kuku wa nyama.*
*(v) Sisi tu**na**panda Mlima Meru.*
*(vi) Watoto wa baba mdogo wa**na**palilia shamba lao.*
*(vii) Ufugaji wa nyuki u**na**waneemesha vijana wa Mzee Hango.*
*(viii) Mwalimu Kabaka a**na**tufundisha tabia njema.*
*(ix) Kabati li**na**lonunuliwa leo li**na**wekwa hapa.*
*(x) Merama a**na**kunywa uji wa ulezi.*

D. Kuandika KWELI au SI KWELI
Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo.
(ii) Andika ubaoni maswali yenye maelezo ya KWELI na SI KWELI.
(iii) Waongoze wanafunzi kujibu maswali hayo kwa mazungumzo kwa kutumia KWELI au SI KWELI
(iv) Kwa kutumia mifano hiyo, waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 D lililopo ukurasa wa **7** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI_KISW.indd 6 7/23/21 3:23 PM

Majibu

(i) KWELI
(ii) KWELI
(iii) SI KWELI
(iv) KWELI
(v) SI KWELI
(vi) SI KWELI
(vii) KWELI
(viii) KWELI
(ix) KWELI
(x) SI KWELI

E. Kupigia mstari vitenzi vikuu na kuandika herufi T chini yake katika sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo la vitenzi vikuu.
(ii) Andika ubaoni au kwenye bangokitita sentensi zenye vitenzi mbalimbali.
(iii) Waongoze wanafunzi kubaini vitenzi vikuu vilivyojitokeza katika sentensi hizo.
(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 E lililopo ukurasa wa **7** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Leo <u>tumecheza</u> mpira kwa furaha kubwa.
T

(ii) Mimi <u>ninawapenda</u> sana baba na mama.
T

(iii) Otaigo <u>ameandika</u> insha kwa mwandiko mzuri sana.
T

(iv) Kisima <u>kimebomoka</u> mara tu baada ya mvua.
T

(v) Wiki ijayo tutakuwa <u>tunafanya</u> mtihani.
T

(vi) Mtendaji wa kijiji alikuwa <u>anagawa</u> pembejeo.
T

(vii) Wanafunzi wa shule yetu <u>walishinda</u> mechi kwa kishindo.
T

(viii) Baba yao atakuwa <u>anapalilia</u> mikorosho.
T

(ix) Nyumbani kwetu <u>tunauza</u> mafuta ya alizeti.
T

(x) Mtoto <u>alianguka</u> vibaya sana.
T

KIONGOZI_KISW.indd 7 7/23/21 3:23 PM

F. Kuoanisha maelezo ya kifungu A na B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi toka kifungu B kwenye nafasi iliyoachwa wazi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo.

(ii) Waongoze wanafunzi kujadili jinsi ya kujibu maswali ya kuoanisha.

(iii) Waongoze wanafunzi kubaini na kurekebisha kasoro zinazojitokeza.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 F lililopo ukurasa wa **8** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) *g*
(ii) *f*
(iii) *h*
(iv) *d*
(v) *l*
(vi) *k*
(vii) *j*
(viii) *a*
(ix) *b*
(x) *e*

Somo la 8: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kuchagua mada za kutungia shairi.

(b) Waongoze wanafunzi kujadili mambo ya kuzingatia katika utunzi wa shairi la kimapokeo mfano mizani, vina, idadi ya mishororo na mkarara/kituo.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga shairi la kimapokeo kwa kuzingatia mambo waliyoyataja.

(d) Sahihisha mashairi yaliyotungwa na kurekebisha makosa yaliyojitokeza.

(e) Waongoze wanafunzi kuchambua maudhui ya mashairi waliyoyatunga.

(f) Rekebisha makosa yanayojitokeza.

(g) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 lililopo ukurasa wa **9** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI_KISW.indd 8 7/23/21 3:23 PM

Somo la 9: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu mashairi ya kisasa. Kumbuka mashairi ya kisasa hayazingatii urari wa vina na mizani wala urari wa idadi ya mishororo katika ubeti. Pia, alama za uandishi katika beti za mashairi haya huwekwa baada ya wazo kukamilika.

(b) Waongoze wanafunzi kujadili kuhusu muundo wa shairi la kisasa.

(c) Waongoze wanafunzi kusoma kwa sauti shairi la kisasa lililopo ukurasa wa **9** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(d) Waongoze wanafunzi kujadili tofauti zilizopo kati ya shairi la kisasa na la kimapokeo.

(e) Waulize wanafunzi maswali yafuatayo:
   (i) Shairi hili linahusu nini?
   (ii) Kila ubeti wa shairi ulilosoma una mishororo mingapi?

(f) Waongoze wanafunzi kujadili lugha ya picha (taswira) iliyotumika katika shairi hilo.

(g) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 7 lililopo ukurasa wa **10** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Somo la 10: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha matumizi ya maneno yafuatayo: *engaenga, hisi, semezana, elekeza, tuliza, huba, hakikisha, hangaisha, guswa* na *muungwana*.

(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya neno mojamoja kama lilivyotumika katika shairi.

(c) Tumia mbinu mbalimbali katika kufundisha msamiati: mfano mbinu ya maelezo, mjadala, maswali na majibu, igizo au mbinu nyinginezo.

(d) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi mbili kwa kila neno kwa mazungumzo kwa kutumia maneno hayo. Andika sentensi hizo ubaoni na uangalie kama ziko sahihi. Washirikishe wanafunzi wazisome kwa sauti.

KIONGOZI_KISW.indd 9 7/23/21 3:23 PM

(e) Tumia mifano kuwaongoza wanafunzi kufanya zoezi la 8 lililopo ukurasa wa **10** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Zingatia kwamba sentensi watakazotunga, zisifanane na zile walizotunga katika mifano ya darasani.

Somo la 11: Miundo

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo.
(b) Andika mifano ya miundo mbalimbali ubaoni.
(c) Waongoze wanafunzi kusoma miundo hiyo kwa sauti; kisha, waitungie sentensi.
(d) Waongoze wanafunzi kurekebisha dosari zinazojitokeza katika sentensi walizozitunga.
(e) Tumia mifano kuwaongoza wanafunzi kufanya zoezi la 9 lililopo ukurasa wa **10** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Somo la 12: Mazoezi ya lugha

A. Kupigia mstari vielezi katika sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa.
(ii) Andika aina mbalimbali za maneno ubaoni.
(iii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi zenye vielezi ndani yake. Ongoza wanafunzi kubaini vielezi kutoka kwenye sentensi zilizotungwa.
(iv) Tumia mfano kuwaongoza wanafunzi wafanye zoezi la 10 A lililopo ukurasa wa **11** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Binamu yangu analima kwa bidii.
(ii) Mtoto wa mjomba anacheza polepole.
(iii) Wanafunzi wameingia darasani.
(iv) Baba mkubwa anaishi Tarime.
(v) Mwalimu atafika saa tatu kamili.
(vi) Hapa pameinuka sana.
(vii) Mama atafika kesho jioni.

KIONGOZI_KISW.indd 10 7/23/21 3:23 PM

(viii) Ndama wataingia zizini.
(ix) Kinyonga anatembea kwa maringo.
(x) Maji ya kunywa yalimwagika mwaaa!

B. Kuandika visawe vya maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya ufafanuzi kuhusu dhana ya visawe kuwa ni maneno tofauti lakini yenye maana sawa.

(ii) Andika maneno mbalimbali ubaoni na visawe vyake kwa kuyachanganya katika orodha.

(iii) Waongoze wanafunzi kuchambua kila neno na visawe vyake.

(iv) Waongoze wanafunzi kutaja maneno na visawe vyake kadiri inavyowezekana.

(v) Waongoze wanafunzi wafanye zoezi la 10 B lililopo ukurasa wa **11** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) tisa
(ii) mtu
(iii) kitenzi/tendo
(iv) jiuzulu/staafu
(v) angika/tundika/aliki
(vi) umri/rika
(vii) adabu/taadhima/itibari
(viii) goli/aguo/ushindi/ramli
(ix) wastani/kiwango/kadiri
(x) taifa/dola/jamhuri

C. Kubadili sentensi kuwa katika hali ya mazoea

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya ufafanuzi kuhusu hali ya mazoea. Kumbuka hali ya mazoea huashiriwa kwa kiambishi **hu-** katika kitenzi katika uyakinishi na kiambishi **ha-** ambacho hutanguliwa na neno **huwa** katika kitenzi katika ukanushi.

KIONGOZI_KISW.indd 11 7/23/21 3:23 PM

(ii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi mbalimbali.
(iii) Andika sentensi walizotunga ubaoni.
(iv) Waongoze wanafunzi kubadili sentensi hizo kuwa katika hali ya mazoea.
(v) Wasaidie wanafunzi kurekebisha makosa yanayojitokeza.
(vi) Tumia mifano kuwaongoza wanafunzi wafanye zoezi la 10 C lililopo ukurasa wa **11** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Watanzania hupenda mpira wa miguu.
(ii) Doto husafiri umbali mrefu kwenda shuleni.
(iii) Mtoto hulia kwa sauti kubwa.
(iv) Nchama hufika ofisini saa mbili asubuhi.
(v) Watoto hucheza mpira kwa bidii.
(vi) Ng'ombe wetu hutoa maziwa mengi.
(vii) Wanafunzi hugawiwa vitabu kwa ajili ya kujisomea.
(viii) Jogoo huwika saa kumi alfajiri.
(ix) Mwajuma huogelea bwawani.
(x) Kitigwa huenda bandarini kuchukua mizigo.

D. Kubadili sentensi kuwa katika wakati ujao

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu wakati ujao.
(ii) Waongoze wanafunzi kuchangia na kuuliza maswali.
(iii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi mbalimbali za Kiswahili katika wakati uliopo na uliopita.
(iv) Andika sentensi walizotunga ubaoni au kwenye bangokitita.
(v) Waongoze wanafunzi kubadili sentensi hizo kuwa katika wakati ujao.
(vi) Waongoze wanafunzi kurekebisha makosa yanayojitokeza.
(vii) Waongoze wanafunzi kujadili matumizi ya vielezi vifuatavyo: leo, jana, kesho na juzi.
(viii) Waongoze wanafunzi kubadili sentensi hii katika wakati ujao.
Mtoto alikutembelea jana.
Mtoto atakutembelea kesho.

KIONGOZI_KISW.indd 12 7/23/21 3:23 PM

(ix) Waongoze wanafunzi wafanye zoezi la 10 D lililopo ukurasa wa **12** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

*(i) Musa a**ta**imba vizuri nyimbo za kwao.*
*(ii) Baba a**ta**endesha gari mpaka nje ya nchi.*
*(iii) Sisi tu**ta**ishi Kijiji cha Nyarero.*
*(iv) Mlevi a**ta**anguka kwenye mtaro.*
*(v) Wao wa**ta**kula wali kesho.*
*(vi) Dagaa wa**ta**pungua sokoni.*
*(vii) Mvua za masika zi**ta**anza kunyesha.*
*(viii) Kilimo cha matunda ki**ta**msomeshea watoto.*
*(ix) Mwanariadha a**ta**tunukiwa medali ya dhahabu.*
*(x) Kidado a**ta**jua kupika ugali.*

E. Kutunga sentensi mbili kwa kila neno zenye maana tofauti

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo.
(ii) Waongoze wanafunzi kutaja maneno yenye maana zaidi ya moja, kisha uyaandike maneno hayo ubaoni.
(iii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi mbalimbali kwa kila neno.
(iv) Waongoze wanafunzi kurekebisha makosa yaliyojitokeza.
(v) Tumia mifano kuwaongoza wanafunzi kufanya zoezi la 10 E lililopo ukurasa wa **12** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(vi) Angalia usahihi wa sentensi za wanafunzi wakati unasahihisha.

F. Kupigia mstari jibu sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya ufafanuzi kuhusu somo utakalofundisha.
(ii) Andika maneno kadhaa sahihi na yasiyo sahihi ubaoni, kisha waongoze wanafunzi kubaini na kupigia mstari neno sahihi kutokana na orodha iliyoandikwa. Hakikisha wanafunzi wanapigia mstari jibu sahihi na kutojaza kwenye nafasi iliyoachwa wazi. Zingatia kuwa hapa mwanafunzi anasisitizwa kusoma na kuelewa maelekezo ya swali.

KIONGOZI_KISW.indd 13 7/23/21 3:23 PM

(iii) Waongoze wanafunzi kurekebisha makosa yaliyojitokeza.
(iv) Waongoze wanafunzi wafanye zoezi la 10 F lililopo ukurasa wa **12 - 13** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) (kitenzi, kivumishi, kiwakilishi, kielezi)
(ii) (kivumishi, kitenzi, kielezi, kiwakilishi)
(iii) (kiunganishi, kitenzi, nomino, kiwakilishi)
(iv) (imenyauka, imekauka, imeungua, imechanua)
(v) (chao, chake, vyake, yake)
(vi) (moja, mbili, pili, chanzoni)
(vii) (yakaniudhi, yaliniudhi, yaliniuzi, yaliniuthi)
(viii) (safi, supu, sufu, sufi)
(ix) (panzi, mende, kinyonga, mbu)
(x) (batamzinga, kanga, batamaji, batabukini)

G. Kukamilisha methali

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja methali wanazozifahamu.
(ii) Andika methali hizo ubaoni.
(iii) Ongeza methali zingine bila kuzikamilisha. Acha nafasi ya kukamilisha mwanzoni au mwishoni mwa kila methali.
(iv) Waongoze wanafunzi kumalizia methali hizo.
(v) Waongoze wanafunzi kurekebisha makosa yaliyojitokeza wakati wa kukamilisha methali.
(vi) Waongoze wanafunzi wafanye zoezi la 10 G lililopo ukurasa wa **13** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) hayazuii maji kuteremka
(ii) hana pa kwenda
(iii) humpiga wako
(iv) baada ya taabu
(v) huitambui ijapo
(vi) Ujana ni moshi
(vii) Walio mbali kwa mbali
(viii) hupasuka msamba

KIONGOZI_KISW.indd 14 7/23/21 3:23 PM

(ix) ndipo pepo zikuapo
(x) Akikalia kigoda

Somo la 13: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo.
(b) Waongoze wanafunzi kujadili mambo ya kuzingatia katika kutunga mashairi ya kisasa.
(c) Waongoze wanafunzi kutunga shairi la kisasa kwa kuzingatia mambo waliyoyataja.
(d) Rekebisha dosari zinazojitokeza.
(e) Waongoze wanafunzi kuchambua maudhui na taswira zinazojitokeza katika shairi.
(f) Waongoze wanafunzi wafanye zoezi la 11 lililopo ukurasa wa **13** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(g) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia vipengele na vigezo vya utunzi wa mashairi ya kisasa.

KIONGOZI_KISW.indd 15 7/23/21 3:23 PM

Sura ya Pili

Utenzi

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kughani utenzi. Pia, atatunga utenzi kwa kuzingatia vina na mizani na kueleza ujumbe wake.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kughani utenzi wa **Teknolojia ya kisasa**
(b) kueleza ujumbe unaopatikana katika utenzi huo
(c) kutunga utenzi

Mahitaji: utenzi wa mfano, matini mbalimbali zenye tenzi, manila na kalamu rashasha

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kufikiri juu ya sifa bainifu za utenzi katika kipengele cha fikiri ukurasa wa **14** wa Kitabu cha Mwanafunzi.
(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya utenzi uliopo ukurasa wa **14 - 15** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Wasome bila kufuatisha vidole wala kutoa sauti.
(c) Waulize wanafunzi maswali yafuatayo:
    (i) Kila ubeti wa utenzi uliousoma una mizani ngapi?
    (ii) Utenzi unahusu nini?
    (iii) Eleza sifa ya kina cha kituo cha beti za utenzi uliousoma.
(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **15** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Wakumbushe wanafunzi kanuni na taratibu sahihi za kusoma kwa sauti.
(b) Toa maelezo mafupi kuhusu usomaji sahihi wa utenzi kwa kuzingatia kiimbo na hisia.

KIONGOZI_KISW.indd 16 7/23/21 3:23 PM

(c) Wakumbushe wanafunzi kuhusu vina, mizani na mishororo. Wataje vina vya mwisho kwa kila ubeti na kuhesabu idadi ya mizani katika kila mstari. Vina ni silabi zinazofanana mwishoni mwa mshororo wa kila ubeti wa utenzi. Mizani ni idadi ya silabi katika mshororo.
(d) Washirikishe wanafunzi kutaja vina vya kila ubeti.
(e) Waongoze wanafunzi kughani utenzi kishairi.
(f) Wakati wanafunzi wanaghani, baini dosari zinazojitokeza na kuzirekebisha.
(g) Wanafunzi warudie kughani kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha matumizi ya msamiati ufuatao: *somo, geua, aali, epesi, sawia, boresha, masafa, utandawazi, ubunifu* na *tija*.
(b) Tumia mbinu mbalimbali, kwa mfano mbinu ya maelezo, mjadala, maswali na majibu, igizo au mbinu nyinginezo.
(c) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya neno mojamoja kama lilivyotumika kwenye utenzi.
(d) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kuzungumza kwa kutumia maneno hayo. Andika sentensi hizo ubaoni na angalia kama ziko sahihi. Washirikishe wanafunzi wazisome kwa sauti.
(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili ukurasa wa **16** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Wasisitize kuwa sentensi watakazotunga zisifanane na zile walizotunga katika mifano darasani.

Somo la 4: Kutegua vitendawili

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutega na kutegua vitendawili wanavyovifahamu.
(b) Tumia mfano uliopo zoezi la 3 kuwaongoza wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa **16** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Wanafunzi wajibu maswali hayo kwa kuzungumza.
(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi hili kwenye madaftari yao.

KIONGOZI_KISW.indd 17 7/23/21 3:23 PM

Majibu

1. *(kaburi)*
2. *(kata ya kuchotea maji)*
3. *(maji)*
4. *(firigisi)*
5. *(mgomba)*
6. *(yai na kifaranga)*
7. *(radi)*
8. *(nungunungu)*
9. *(mwiko wa kupikia ugali)*
10. *(kwapa)*

Somo la 5: Mazoezi ya lugha

A. Kuandika umoja au wingi wa maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu umoja na wingi.

(ii) Tumia mifano iliyopo katika zoezi la 4 A lililopo ukurasa wa **17** katika Kitabu cha Mwanafunzi kuwaelekeza wanafunzi dhana ya umoja na wingi. Unaweza kuongeza mifano mingine.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 A lililopo ukurasa wa **17** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu

(i) magego
(ii) mjasiriamali
(iii) vyote
(iv) ubeti
(v) mishumaa
(vi) mdokozi
(vii) mizabibu
(viii) kitovu
(ix) vichaa
(x) kope

B. Kuandika sentensi katika wakati uliopita

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja nyakati mbalimbali, kwa mfano, wakati uliopo, ujao na uliopita.

(ii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kuzingatia nyakati hizo.

(iii) Wakumbushe kuwa kiambishi kinachoonesha wakati uliopita katika kitenzi ni -li- katika uyakinishi na -ku- katika ukanushi.

KIONGOZI_KISW.indd 18 7/23/21 3:23 PM

(iv) Andika ubaoni sentensi zilizopo zoezi la 4 B ukurasa wa **17** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(v) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi zilizoandikwa ubaoni.

(vi) Waongoze wanafunzi kubadili sentensi kuwa katika wakati uliopita. Tumia mifano iliyopo zoezi la 4 B lililopo ukurasa wa **17** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(vii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 B lililopo ukurasa wa **17** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu

(i) Serikali ilitoa mikopo ya fedha kwa wajasiriamali wadogo.
(ii) Mjomba alitunga utenzi kuhusu maadili ya jamii.
(iii) Mwandishi aliikosoa jamii kwa kuendekeza imani potofu.
(iv) Mwalimu hakutunga mtihani wa muhula wa pili.
(v) Dereva aliendesha gari kwa umakini mkubwa.
(vi) Kiranja hakusimamia usafi wa mazingira ya shule.
(vii) Wanakijiji walichagua viongozi wa kijiji chao.
(viii) Wanafunzi walichimba shimo la takataka shuleni.
(ix) Wanachuo walisafiri kuelekea mbuga ya wanyama.
(x) Kwaya ya shule yetu ilitumbuiza kwenye Sherehe za Muungano.

C. Kuandika kinyume cha neno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo.

(ii) Andika ubaoni maneno machache bila vinyume vyake.
Mfano: *nadra* _____
zika _____

(iii) Waongoze wanafunzi kutaja kinyume cha kila neno kwa maneno yaliyoandikwa ubaoni.

(iv) Andika ubaoni majibu yaliyotajwa na wanafunzi.

(v) Angalia usahihi wa majibu hayo.

(vi) Tumia mifano iliyopo zoezi la 4 C ukurasa wa **18** kuwaongoza wanafunzi kufanya zoezi la 4 C lililopo ukurasa wa **18** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

KIONGOZI_KISW.indd 19 7/23/21 3:23 PM

Majibu

(i) *nusurika/salimika*
(ii) *tabasamu/cheka*
(iii) *fukuza*
(iv) *mchoyo*
(v) *binafsisha*
(vi) *ujinga*
(vii) *dhaifu/legevu/legelege*
(viii) *pinga/kataa*
(ix) *nafuu/rahisi*
(x) *kosekana/adimika*

D. Kujaza neno sahihi katika sehemu iliyoachwa wazi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo.
(ii) Waongoze wanafunzi kujaza neno sahihi katika sentensi kwa kutumia mifano iliyopo zoezi la 4 D ukurasa wa **18** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 D lililopo ukurasa wa **18 - 19** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) *umezaa*
(ii) *ambao*
(iii) *ndiye*
(iv) *hauna*
(v) *angalikamatwa*
(vi) *ingawa*
(vii) *hazifai*
(viii) *wanapalilia*
(ix) *mizuri*
(x) *alikuwa*

E. Kubadili sentensi kuwa katika kauli halisi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya jumla kuhusu namna ya kubadili sentensi za kauli taarifa kuwa katika kauli halisi. Waambie wanafunzi kuwa kauli halisi ni maneno yanayosemwa na msemaji mwenyewe. Maneno hayo huwa na alama za fungua na funga semi.
(ii) Tumia mifano iliyopo katika zoezi la 4 E ukurasa wa **19** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 E lililopo ukurasa wa **19** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI_KISW.indd 20 7/23/21 3:23 PM

Majibu

(i) Mwalimu amesema, "Nendeni upesi."

(ii) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilisema, "Mnasajili laini za simu zenu ili kuzuia uhalifu."

(iii) Bwana Afya aliuliza, "Kuna umuhimu gani wa kuchemsha maji ya kunywa?"

(iv) Mwanafunzi mwenzangu alisema, "Kalamu yako inaandika vizuri sana."

(v) "Wewe ni nani?" Mgeni aliuliza.

(vi) Waziri alisema, "Ajira huchochea ukuaji wa uchumi."

(vii) "Nidhamu ni msingi wa maendeleo ya taaluma shuleni," mwalimu alisema.

(viii) Mtabiri wa hali ya hewa alisema, "Mwaka ujao kutakuwa na mvua nyingi."

(ix) Kiranja alisema, "Kila mwanafunzi atatakiwa kuja na ufagio kwa ajili ya usafi."

(x) "Unaumwa ugonjwa wa malaria," daktari alimwambia mgonjwa.

Zingatia: Maelekezo yanayomtaja mtoa taarifa halisi yanaweza kutokea kabla au baada ya kauli halisi.

Somo la 6: Kazi ya kufanya

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo.

(b) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 lililopo ukurasa wa **19** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(c) Toa maelekezo kwa wanafunzi kuhusu mambo ya kuzingatia wakati wa kutembelea maktaba.

(d) Sisitiza lengo la kwenda kutembelea maktaba na kufuata sheria na taratibu za maktaba.

(e) Waongoze wanafunzi kuwasilisha kwa njia ya maandishi maudhui ya tenzi walizozisoma.

(f) Kusanya kazi zote za wanafunzi na weka kwenye mkoba wa kazi.

KIONGOZI_KISW.indd 21 7/23/21 3:23 PM

Somo la 7: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Ongoza mazungumzo kuhusu somo la utungaji.

(b) Waongoze wanafunzi kujadili kuhusu mada ya utungaji kama ilivyobainishwa katika zoezi la 6 lililopo ukurasa wa **19** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuwaongoza kwa kuwauliza maswali yafuatayo:

(i) Mmomonyoko wa maadili ni nini?

(ii) Mambo gani husababisha mmomonyoko wa maadili katika jamii?

(iii) Athari zipi zinatokana na mmomonyoko wa maadili katika jamii?

(iv) Mbinu gani zitumike kuzuia mmomonyoko wa maadili katika jamii?

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 lililopo ukurasa wa **19** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

(d) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia usahihi katika vina na mizani, alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, mtiririko mzuri wa mawazo na matumizi ya herufi kubwa.

KIONGOZI_KISW.indd 22 7/23/21 3:23 PM

Sura ya Tatu

Ngonjera

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kutamba, kutafsiri lugha ya picha na kueleza ujumbe wa ngonjera aliyoitamba. Vilevile, atajifunza kutunga ngonjera na atafanya mazoezi mbalimbali ya lugha ili kuimarisha ujuzi wake katika lugha ya Kiswahili.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kusoma ngonjera inayohusu kuku
(b) kutamba ngonjera kwa sauti ya utambaji
(c) kubaini wahusika walio katika ngonjera
(d) kubaini lugha ya picha iliyotumika katika ngonjera
(e) kutunga ngonjera

Mahitaji: vitu halisi, picha (ya kawaida na ya mguso), vitendo, bangokitita na kalamu rashasha

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kufikiri juu ya tofauti kati ya ngonjera na shairi katika kipengele cha *fikiri* kilichopo ukurasa wa **20** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya ngonjera kuhusu **Kuku** iliyopo ukurasa wa **20 - 22** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.
(c) Waongoze wanafunzi kujibu swali hili:
Kuku asiyetaga anawakilisha nini?
(d) Waongoze wanafunzi waeleze ngonjera waliyosoma inahusu nini.
(e) Waongoze wanafunzi kujadili kuhusu lugha ya picha (taswira) iliyotumika katika ngonjera hiyo.
(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **22** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI_KISW.indd 23 7/23/21 3:23 PM

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu ngonjera ya **Kuku**. Wakumbushe wanafunzi kanuni na taratibu za kusoma ngonjera kwa sauti.

(b) Wakumbushe wanafunzi kuhusu vina, mizani na mishororo. Wataje vina vya kila ubeti na kuhesabu idadi ya mizani katika kila mstari. Vina ni silabi za mwisho katika kila kipande cha mshororo katika ubeti wa ngonjera, shairi au utenzi. Mizani ni idadi ya silabi katika mshororo wa ngonjera, shairi au utenzi.

(c) Washirikishe wanafunzi kutaja vina kwa kila ubeti.

(d) Chagua wahusika: Hekima na Majivuno na kuwapa uhusika katika kusoma ngonjera. Kumbuka kuzingatia jinsi zao.

(e) Toa muda mfupi kwa kila mhusika kusoma kimya sehemu yake.

(f) Waongoze wanafunzi kutamba ngonjera kwa kuzingatia uhusika na kanuni za kutamba kwa sauti. Wanaweza kutamba ngonjera hii zaidi ya mara moja kwa kubadili wahusika.

(g) Wakati wanafunzi wakitamba, baini dosari zinazojitokeza na uzisahihishe.

(h) Waongoze wanafunzi kutamba ngonjera kwa usahihi. Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(i) Wanafunzi warudie kutamba ngonjera kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha maana na matumizi ya maneno yafuatayo: *kuku, taga, kiota, hujuma, maalumu, piku* na *totoa*.

(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya neno mojamoja.

(c) Nakili ubaoni au kwenye bangokitita jedwali lililopo zoezi la pili ukurasa wa **22 - 23** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(d) Waongoze wanafunzi kuunda maneno sahihi kutokana na jedwali hilo. Rekebisha makosa yatakayojitokeza na yaandike

KIONGOZI_KISW.indd 24 7/23/21 3:23 PM

maneno hayo ubaoni, kwa mfano, *KIOTA*.

(e) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa kuzungumza. Andika sentensi hizo ubaoni.
Mfano: Kuku *wetu wote wametaga mayai mengi.*

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **22 - 23** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao. Sentensi ziwe tofauti na zilizotolewa mfano.

Somo la 4: Mazoezi ya lugha

A. Kuandika sentensi katika umoja

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi zote kumi zilizopo kwenye zoezi la 3 A lililopo ukurasa wa **23** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuchagua wanafunzi au safu tofautitofauti kusoma sentensi hizi.

(ii) Waongoze wanafunzi kujibu swali la kwanza kama mfano. Rekebisha papo hapo dosari inapojitokeza.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 A lililopo ukurasa wa **23** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Ngonjera ni shairi la kujibizana lenye kufuata kanuni za vina na mizani.

(ii) Mhusika ni sifa muhimu ya ngonjera.

(iii) Kazi ya fasihi inaeleza tatizo lililopo katika jamii.

(iv) Mhusika anatamba ngonjera.

(v) Timu ya shule yetu inafungwa na timu ya shule ya jirani.

(vi) Mwanafunzi anatunga ngonjera kwa kushirikiana na mwalimu.

(vii) Mfanyakazi anakwenda kumtembelea mgonjwa hospitalini.

(viii) Kaka yangu amepata ushindi katika Shindano la Kurusha Mkuki.

(ix) Babu yangu ni mashuhuri kwa kuwa ni mkwezi mzuri.

(x) Mshindi atapewa medali ya dhahabu.

KIONGOZI_KISW.indd 25 7/23/21 3:23 PM

B. Kutumia irabu kujaza nafasi zilizoachwa wazi kuunda maneno sahihi ya Kiswahili

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya somo litakalofundishwa.

(ii) Waongoze wanafunzi kutaja irabu zote na uziandike ubaoni.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya swali la kwanza kama mfano. Andika jibu hilo ubaoni kwa kuzingatia maelekezo ya swali.

Mfano: Sh__mr__sh__mr__ - shamrashamra

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 B lililopo ukurasa wa **23** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu

(i) shamrashamra
(ii) vigelegele
(iii) malumbano
(iv) utenzi/utunzi
(v) majigambo
(vi) fanani/fununu/fanana/fanano
(vii) hadhira/hadhara/ hadhari
(viii) ngonjera
(ix) mandhari
(x) bapa/bopa/bopo

Tanbihi: Angalia majibu mengine sahihi yatakayotolewa na wanafunzi.

C. Kukamilisha chemshabongo kwa kufuata maelekezo yaliyotolewa kwenye herufi

Hatua za ufundishaji

(i) Nakili fumbo kwenye bangokitita au ubaoni.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma maelezo yaliyopo kwenye herufi a hadi d kwa sauti.

(iii) Waongoze kutoa majibu kwa swali moja kama mfano.

(iv) Andika herufi moja kwa kila chumba kwa kuzingatia uelekeo wa herufi hiyo kwa herufi kubwa.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 C lililopo ukurasa wa **24** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI_KISW.indd 26 7/23/21 3:23 PM

Majibu

a **b**

T	A	M	B	A
E	I		M	L
M		A		A
B	G		R	M
E	L	E	Z	A

c **d**

D. Kujaza nafasi zilizoachwa wazi

Hatua za ufundishaji

(i) Waeleze wanafunzi muundo wa sentensi zilizopo kwenye zoezi la 3 D lililopo ukurasa wa **24** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yote kwa mazungumzo.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi kwa kutumia mifano iliyopo kwenye zoezi la 3 D lililopo ukurasa wa **24** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 D lililopo kwenye ukurasa wa **24** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Kughani ni kwa shairi/utenzi, kutamba ni kwa ngonjera/hadithi.

(ii) Saa ni ya muda. Taa ni ya mwanga.

(iii) Miwani ni ya macho. Mkufu ni wa shingo.

(iv) Macho ni ya kuona. Pua ni ya kunusa.

(v) Pete ni ya kidole. Viatu ni vya miguu.

(vi) Kiota ni cha ndege. Mzinga ni wa nyuki.

(vii) Simu/barua ni ya mawasiliano. Kamera ni ya picha.

(viii) Vinywaji ni vya kunywa. Chakula ni cha kula.

(ix) Mwanafunzi/mwalimu ni wa shule. Mgonjwa ni wa hospitali.

(x) Pazia ni la dirisha. Shuka ni la kitanda.

Tanbihi: Angalia majibu mengine sahihi yatakayotolewa na wanafunzi.

KIONGOZI_KISW.indd 27 7/23/21 3:23 PM

E. Kubadili sentensi kuwa katika hali timilifu

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja viambishi vya nyakati tofautitofauti, kwa mfano **-li-** wakati uliopita, **-ta-** wakati ujao na **-na-** wakati uliopo.

(ii) Waongoze wanafunzi kutambua kiambishi kinachotambulisha hali timilifu kuwa ni **-me-** kwenye kitenzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi kwa kutumia mfano uliopo zoezi la 3 E ukurasa wa **24** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 E lililopo ukurasa wa **24 - 25** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Wahitimu wote wamemaliza kufanya mitihani yao.

(ii) Sote tumepatiwa namba zetu za kufanyia mtihani.

(iii) Kila mtahiniwa amebandika namba yake ya mtihani kwenye dawati lake.

(iv) Wanafunzi wamepewa kadi za mwaliko wa Mahafali ya Darasa la Saba.

(v) Walimu wote wamehudhuria mahafali yetu.

(vi) Ukumbi umepambwa kwa mawaridi ya kila rangi.

(vii) Ngoma ya Kimasai imetumbuiza waalikwa wote.

(viii) Wavulana wamevaa mashati meupe na suruali nyeusi.

(ix) Wazazi na walezi wameandaa mashada ya kutuvisha.

(x) Wageni wameonesha kadi za mwaliko mlangoni kabla ya kuingia ukumbini.

Somo la 5: Kazi ya kufanya

Hatua za ufundishaji

(a) Wagawe wanafunzi katika makundi mawili yaliyo sawa kwa kuzingatia jinsi zao.

(b) Waongoze wanafunzi katika makundi yao kupata wahusika wa ngonjera, yaani Uledi na Jeni.

KIONGOZI_KISW.indd 28 7/23/21 3:23 PM

(c) Wape muda wanafunzi kujiandaa kwa kulingana na wahusika kwa ajili ya kutamba ngonjera.
(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa **25 - 26** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(e) Hakikisha kila mhusika anashiriki ipasavyo na wapongeze pale wanapofanya vizuri.

Somo la 6: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo.
(b) Waongoze wanafunzi kutaja mada wanazozipenda na uziandike ubaoni.
(c) Toa maelezo jinsi ya kutunga ngonjera. Kumbuka kila mstari mmoja hukadiriwa kuwa na mizani nane au kumi na sita.
(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 lililopo ukurasa wa **26** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwa kuandika kwenye madaftari yao. Kumbuka ubeti wa mwisho uwe wa makubaliano ya pande zote.
(e) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, idadi ya mizani katika mshororo na mwandiko mzuri.
(f) Baada ya kusahihisha, chagua kazi iliyoandikwa vizuri, wanafunzi waisome darasani kwa sauti.

KIONGOZI_KISW.indd 29 7/23/21 3:23 PM

Sura ya Nne

Vitendawili

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kutafsiri lugha ya picha katika vitendawili. Pia, ataendelea kutega na kutegua vitendawili ili kujijengea ujuzi wa kuwa mbunifu na mdadisi. Vilevile, mwanafunzi atajenga umahiri wa kutumia lugha ya mafumbo.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kutafsiri lugha ya picha katika vitendawili
(b) kutega na kutegua vitendawili
(c) kutunga hadithi kwa kutumia vitendawili

Mahitaji: vitu halisi, mazingira halisi, picha (ya kawaida na ya mguso), chati, bangokitita, diski ya igizo (sidii ya igizo), projekta, televisheni, deki, kinyonyi na kompyuta

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kufikiri juu ya lugha inayotumika katika vitendawili katika kipengele cha *fikiri* ukurasa wa **27** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari iliyopo ukurasa wa **27 - 29** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kidole wala kutoa sauti.
(c) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:
    (i) Nani alidokoa vyakula vya majirani?
    (ii) Nani alifanikiwa kumkamata Ranginyingi?
(d) Waongoze wanafunzi kujadili picha iliyopo ukurasa wa **29** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(e) Waongoze wanafunzi kusimulia habari waliyoisoma kwa maneno machache.
(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza ukurasa wa **30** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

KIONGOZI_KISW.indd 30 7/23/21 3:23 PM

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo.

(b) Wakumbushe wanafunzi alama za uandishi kwa kuuliza maswali.

(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji sahihi kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi sahihi ya alama za uandishi na kusoma kwa hisia.

(d) Waongoze wanafunzi kusoma mmojammoja kwa zamu, bila kujali jinsi zao na uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma kadiri muda utakavyoruhusu.

(e) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha msamiati ufuatao: *ujalunga, zingira, mdokozi, pindukia, ufumbuzi, nena, nyata, kigoda, masafa* na *maovu* kwa kutumia mbinu ya maelezo, picha na maigizo.

(b) Andika maneno hayo ubaoni. Waongoze wanafunzi kusoma neno mojamoja; kisha, watamke sauti zinazounda maneno hayo.

(c) Tunga sentensi kwa kutumia maneno hayo, kisha waongoze wanafunzi kueleza maana za maneno waliyoyatungia sentensi. **Mfano:** Waigizaji wote walijitambulisha jukwaani. Neno "jukwaa" lina maana gani?

(d) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa kuzungumza. Andika sentensi hizo ubaoni.

(e) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga.

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **30** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazotunga siyo zile zilizotolewa mfano.

KIONGOZI_KISW.indd 31 7/23/21 3:23 PM

Somo la 4: Vitendawili

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutega na kutegua vitendawili wanavyovifahamu.
Mfano: Wakati wote wamejiandaa kupigana. (katani/mkonge)

(b) Waongoze wanafunzi kwa kutumia maelezo, picha na mifano kutega na kutegua vitendawili. (Zingatia majibu kulingana na mazingira wanayoishi wanafunzi).

(c) Waongoze wanafunzi kujadili picha mbalimbali; kisha, kutega vitendawili vinavyotokana na picha hizo.

(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 A, B, C na D lililopo ukurasa wa **30 - 32** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu: Zoezi la 3 A

(i) *moto*
(ii) *kibatari/chemli*
(iii) *kujikwaa*
(iv) *uyoga*
(v) *mchi*
(vi) *nazi na mkwezi*
(vii) *fedha*
(viii) *kujikwaa*
(ix) *tui la nazi na maziwa*
(x) *sindano*
(xi) *utoto, ujana, uzee*

Majibu: Zoezi la 3 B

(i) Kinyonga:
- *Akitembea huringa hata akiwa hatarini.*
- *Hujihami bila silaha.*
- *Tajiri wa rangi.*
- *Huuawa na uzazi wake.*

(ii) Moto:
- *Adui tumemzingira lakini hatumuwezi.*

KIONGOZI_KISW.indd 32 7/23/21 3:23 PM

- *Adui yangu ni mharibifu lakini bado namhitaji.*
- *Kidonda cha mzungu hatui nzi.*
- *Mwarabu wangu mkali hana panga wala kisu.*
- *Viti vyote nakalia isipokuwa hicho.*

(iii) Kifo:
- *Akimchukua hamrudishi.*
- *Hachagui wala hashauriwi.*
- *Kila mtu atapitia mlango huu.*

(iv) Maji:
- *Nimempiga mwanangu lakini sijamuumiza.*
- *Wanangu hawapandi mlima bali huteremka daima.*
- *Nimezaliwa mlimani, nikafunikwa majani, jua likanipa joto, daima naenda mbele siwezi kurudi nyuma.*

Majibu: Zoezi la 3 C

(i) Muwa:
- *Niliwachinjia wanangu ng'ombe wakala nyama wakapanda mkia, ukaota ukawa ng'ombe tena.*
- *Nakunywa mchuzi, nyama natupa.*

(ii) Mgomba:
- *Huuawa na uzazi wake.*
- *Ukimkata shingo leo, kesho anayo nyingine.*
- *Ameanguka na makoti yake.*

(iii) Mhindi:
- *Akibeba watoto wake hawezi kuwashusha.*
- *Babu amelala ndani ndevu nje.*
- *Teketeke huzaa gumugumu, gumugumu huzaa teketeke.*

(iv) Mvua:
- *Kilio chake kwetu ni kicheko.*
- *Kulia kwake furaha kwetu.*
- *Nimefagia uwanja wangu kaja miguu mirefu kautibua.*

KIONGOZI_KISW.indd 33 7/23/21 3:23 PM

Majibu: Zoezi la 3 D

[1]B	I	[2]S	I			[3]F	
O		I				I	
G		[4]N	A	N	A	S	I
A		D				I	
		A					
		N		[5]M	A	J	I
[6]N	D	O	T	O			
J				[7]Y	A	I	
I				O			
A							

Somo la 5: Mazoezi ya lugha

A. Kuandika wingi wa maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu umoja na wingi.

(ii) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 4 A lililopo ukurasa wa **32** katika Kitabu cha Mwanafunzi kuwaelekeza wanafunzi dhana ya umoja na wingi.

(iii) Tumia mifano mingi kulingana na mazingira ili kuelezea dhana ya wingi na umoja.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 A lililopo ukurasa wa **32 - 33** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu

(i) televisheni
(ii) wakarimu
(iii) mananasi
(iv) ukatili
(v) chupa
(vi) giza
(vii) mbarika/mibarika
(viii) nyuzio
(ix) mioto
(x) wanawali

KIONGOZI_KISW.indd 34 7/23/21 3:23 PM

B. Kukanusha sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kufafanua dhana ya ukanushi.

(ii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi zilizo katika uyakinishi. Andika sentensi hizo ubaoni; kisha, washirikishe wanafunzi wazikanushe. Andika ubaoni majibu ya wanafunzi; kisha, washirikishe kurekebisha makosa.

(iii) Tumia mifano kuwaongoza wanafunzi kufanya zoezi la 4 B lililopo ukurasa wa **33** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Mwanafunzi hajaenda kucheza mpira.
(ii) Liboli si kijana mvivu.
(iii) Jembe huwa halimtupi mkulima.
(iv) Mwanajeshi hajaenda vitani.
(v) Msafiri hakuisahau bahasha juu ya meza.
(vi) Mwalimu hamwadhibu mwanafunzi.
(vii) Kinyume cha msichana si kigori.
(viii) Mbuzi hajatoroka zizini.
(ix) Bibi hakugombea ubunge wa viti maalumu.
(x) Chakula hiki hakina chumvi nyingi sana.

C. Kuandika wingi wa sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kujadili dhana ya umoja na wingi katika lugha ya Kiswahili.

(ii) Tumia mifano kuwaongoza wanafunzi kubadili sentensi zilizo katika umoja kuwa katika wingi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 C lililopo ukurasa wa **33** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Watoto wa Maria walichelewa shuleni.
(ii) Kuku wetu wameangua vifaranga.
(iii) Wazazi wamewalipia watoto wao ada za shule.
(iv) Wanafunzi wanachezea gololi.

KIONGOZI_KISW.indd 35 7/23/21 3:23 PM

(v) Kalamu za baba haziandiki kabisa.
(vi) Waandishi wamesoma magazeti.
(vii) Mitaa hii ina miti mikubwa sana.
(viii) Vyakula vilivyopikwa na mama ni vitamu.
(ix) Mipira yao inadunda sana.
(x) Wanafunzi wamewapigia simu wazazi wao.

D. Kuandika neno ambalo ni tofauti na mengine

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya somo.
(ii) Tumia mifano kuwaongoza wanafunzi kuandika neno ambalo ni tofauti na mengine katika orodha ya maneno yaliyotolewa.
(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 D lililopo ukurasa wa **34** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) yai
(ii) mbunge
(iii) muwa
(iv) mkeka
(v) kichuguu
(vi) chuma
(vii) mkonga
(viii) kitabu
(ix) twiga
(x) mchungwa

E. Kuandika sentensi katika mtiririko sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelekezo kuhusu somo utakalofundisha.
(ii) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi zilizopo ukurasa wa **34** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(iii) Waulize wanafunzi kama wamegundua kosa lolote wakati wanasoma sentensi hizo.
(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 E lililopo ukurasa wa **34** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Mwajuma huamka asubuhi na mapema.
(ii) Hupata kifunguakinywa.
(iii) Huingia darasani saa moja na nusu.

KIONGOZI_KISW.indd 36 7/23/21 3:23 PM

(iv) Humsikiliza mwalimu kwa makini.
(v) Hujibu maswali kwa usahihi.
(vi) Hupeleka madaftari ofisini kwa mwalimu wake.
(vii) Husimama mstarini tayari kwa kwenda nyumbani.
(viii) Huingia nyumbani akionekana mwenye uchovu.
(ix) Hula chakula cha jioni.
(x) Hupanda kitandani kulala.

Somo la 6: Kazi ya kufanya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kupitia vitabu vya madarasa ya nyuma na kuchambua vitendawili vyote vilivyotumika katika vitabu hivyo.
(b) Waongoze wanafunzi kukusanya vitendawili vinavyotumika katika mazingira ya shuleni.
(c) Waongoze wanafunzi kuandaa orodha ya vitendawili.
(d) Waongoze wanafunzi kufanya kazimradi hiyo kwa mashindano ili kupata vitendawili vingi zaidi.

Somo la 7: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo ya somo.
(b) Waongoze wanafunzi kutaja mambo muhimu ya kuzingatia katika utungaji na yaandike ubaoni.
(c) Waongoze wanafunzi kujadili mambo ya kuzingatia katika utungaji wa hadithi kwa kutumia vitendawili.
(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 lililopo ukurasa wa **34** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(e) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno na herufi kubwa. Zingatia usahihi wa matumizi ya nafsi, nyakati na usahihi wa vitendawili vilivyotungiwa hadithi.
(f) Baada ya kusahihisha, chagua hadithi iliyoandikwa vizuri na wanafunzi, kisha waongoze waisome darasani kwa sauti. Waulize maswali machache yanayohusu maudhui ya hadithi hiyo.

KIONGOZI_KISW.indd 37 7/23/21 3:23 PM

Sura ya Tano

Tutumie methali zetu

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kueleza mafunzo yatokanayo na methali. Pia, atajifunza kutumia methali katika miktadha mbalimbali.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kueleza mafunzo yanayopatikana katika methali
(b) kutumia methali katika miktadha mbalimbali

Mahitaji: vitu halisi, chati za methali, bangokitita, kalamu rashasha na picha (za kawaida na za mguso)

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kufikiri kuhusu kazi za methali katika jamii kwenye kipengele cha *fikiri* ukurasa wa **35** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari ya **Mchelea mwana kulia hulia yeye** iliyopo ukurasa wa **35 - 36** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.
(c) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:
    (i) Subira alipata malezi ya namna gani toka kwa wazazi wake?
    (ii) Subira alipomaliza elimu ya msingi alichaguliwa kwenda wapi?
(d) Waongoze wanafunzi kusimulia habari waliyoisoma kwa maneno machache.
(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **37** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo. Eleza unachotarajia kifanyike katika somo hili.
(b) Wakumbushe wanafunzi kuhusu alama za uandishi kwa kuwauliza maswali.

KIONGOZI_KISW.indd 38 7/23/21 3:23 PM

(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi ya alama za uandishi, na kusoma kwa hisia.

(d) Waongoze wanafunzi mmojammoja kusoma kwa zamu, bila kujali jinsi zao wala uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma. Baini dosari zinazojitokeza wakati wanafunzi wanaposoma na uzirekebishe.

(e) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(f) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha msamiati ufuatao: *simanzi, lindi, sihi, dekeza, kera, kanya, beza, kijicho, kengeuka* na *radhi* kwa kutumia mbinu ya maelezo, vitu halisi, picha na maigizo.

(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome. Waongoze kueleza maana ya neno mojamoja.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kuzungumza kwa kutumia maneno hayo. Andika sentensi hizo ubaoni.

(d) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **37** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazotunga hazifanani na zile zilizotolewa kama mifano na zilizotumika kitabuni.

Somo la 4: Methali

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu methali.

(b) Waongoze wanafunzi kutaja methali wanazozifahamu.

(c) Ziandike ubaoni methali hizo.

(d) Waongoze wanafunzi kutoa methali zenye maana sawa, kumalizia methali na kuoanisha methali zenye maana sawa kwa kutumia mifano iliyopo zoezi la 3 A, B, na C ukurasa wa **37 - 39** katika Kitabu cha Mwanafunzi kama mifano.

KIONGOZI_KISW.indd 39 7/23/21 3:23 PM

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 A, B na C lililopo ukurasa wa **37 - 39** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu: Zoezi la 3 A

(i) *Mgonjwa haulizwi uji/Mwenye macho haambiwi tazama.*
(ii) *Akumulikaye mchana, usiku atakuchoma.*
(iii) *Harakaharaka haina baraka.*
(iv) *Kupata si kwa werevu, kukosa si kwa ujinga.*
(v) *Yaliyopo Unguja na Pemba yapo.*
(vi) *Hakuna ziada mbovu.*
(vii) *Mtaka yote kwa pupa, hukosa yote.*
(viii) *Ivumayo haidumu.*
(ix) *Sikio la kufa halisikii dawa.*
(x) *Baniani mbaya kiatu chake dawa.*

Tanbihi: Angalia majibu mengine sahihi yatakayotolewa na mwanafunzi.

Majibu: Zoezi la 3 B

(i) *marejeo ngamani*
(ii) *ya tatu mpe jembe akalime*
(iii) *na wake huliwa*
(iv) *ni wakali pia*
(v) *huvuna ufukara*
(vi) *ukamtia mkono kinywani*
(vii) *kifundo*
(viii) *huliwa na mfugaji*
(ix) *zilimshinda fisi*
(x) *hasara ya mwili*

Majibu: Zoezi la 3 C

(i) *e*
(ii) *f*
(iii) *a*
(iv) *b*
(v) *g*
(vi) *i*
(vii) *c*
(viii) *h*
(ix) *j*
(x) *d*

Somo la 5: Imla

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo hili. Sisitiza wanafunzi waandike imla kwa hati ya wima na ya kuunga. Pia, wazingatie alama za uandishi.

KIONGOZI_KISW.indd 40 7/23/21 3:23 PM

(b) Wasomee wanafunzi habari ifuatayo kwa kasi ya kawaida. Wanafunzi wasikilize bila kuandika.

"Mama!" Alisikika Kibibi akimwita mama yake aliyekuwa jikoni. "Njoo huku kuna mgeni." Mama yake alitoka haraka na kuelekea sebuleni. Alipofika sebuleni, alikutana uso kwa uso na mdogo wake aliyepotezana naye siku nyingi. Mama Kibibi alipigwa na mshangao. Lo! Alimkumbatia mdogo wake kwa furaha. Alimuuliza mdogo wake, "Umepotelea wapi mdogo wangu? Hatutafutani!" Mdogo wake alimjibu, "Tulia dada, nitakwambia kila kitu."

(c) Wasomee tena mara ya pili kwa kufuata alama za uandishi huku wakiandika kwenye madaftari yao.

(d) Wasomee taratibu huku wao wakifuatisha na kuhakiki kile walichokiandika.

(e) Kusanya madaftari papo hapo na sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, matumizi ya alama za uandishi, matumizi ya herufi kubwa na hati ya wima ya kuunga na usafi.

Somo la 6: Mazoezi ya lugha

A. Kuoanisha maneno ya sehemu A na maana zake kutoka sehemu B na kutunga sentensi moja kwa kila neno kutoka sehemu A

Hatua za ufundishaji

(i) Wagawe wanafunzi katika makundi mawili yenye mchanganyiko wa wasichana na wavulana.

(ii) Waongoze wanafunzi katika makundi kusoma sehemu A na sehemu B.

(iii) Kundi moja wasome maneno ya sehemu A na kundi jingine wasome maana zake kutoka sehemu B.

(iv) Tumia mifano ya sentensi zilizopo zoezi la 4 A kuwaongoza wanafunzi kuoanisha maneno na maana zake.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 A lililopo ukurasa wa **39 - 40** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Swali la "vi" na "vii" yametumika kama mifano.

KIONGOZI_KISW.indd 41 7/23/21 3:23 PM

Majibu

(i) *e*
(ii) *a*
(iii) *f*
(iv) *b*
(v) *d*

B. Kuchagua neno linalofaa kutoka katika mabano ili kukamilisha sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo.

(ii) Toa mifano ya kuchagua neno sahihi kutoka kwenye mabano na kujaza katika nafasi zilizoachwa wazi.

(iii) Tumia mifano kuwaongoza wanafunzi kufanya zoezi la 4 B lililopo ukurasa wa **40** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) *sufu*
(ii) *ufahari*
(iii) *yanaudhi*
(iv) *puu!*
(v) *chumvi*
(vi) *uhamisho*
(vii) *alitweta*
(viii) *msongo*
(ix) *mkongojo*
(x) *alipaa*

C. Kuchagua maana moja iliyo sahihi kukamilisha semi.

Hatua za ufundishaji

(i) Andika mfano wa swali la kuchagua ubaoni na uwaongoze wanafunzi kulijibu kwa kujaza herufi ya jibu sahihi.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 C lililopo ukurasa wa **41 - 42** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) *b*
(ii) *a*
(iii) *c*
(iv) *c*
(v) *a*
(vi) *c*
(vii) *d*
(viii) *b*
(ix) *a*
(x) *b*

KIONGOZI_KISW.indd 42 7/23/21 3:23 PM

D. Kubainisha nomino katika sentensi kwa kuzipigia mstari

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja aina mbalimbali za nomino.

(ii) Waeleze wanafunzi kuwa nomino ni aina ya neno linalotaja jina la kitu, mahali, mtu au hali. Pia, waeleze kuwa nomino zimegawanyika katika aina nne kama ifuatavyo:

- **Nomino za pekee.** Mifano ni: majina ya watu, Mungu, siku, mwezi na majina ya sehemu
- **Nomino za kawaida.** Mifano ni: kalamu, kitabu na mtu
- **Nomino za dhahania.** Mifano ni: hewa, upendo na njaa
- **Nomino za jumla.** Mifano ni: kikosi, jeshi na kwaya

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 D lililopo ukurasa wa **42 - 43** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Darasa letu lina madawati ya kutosha.
(ii) Asante sana Mwanaisha.
(iii) Shambani kuna mazao mengi.
(iv) Watoto wanaimba wimbo mzuri sana.
(v) Maendeleo ni muhimu katika jamii yoyote.
(vi) Anakula wali kila siku.
(vii) Yeye ni mfanyakazi.
(viii) Amenunua viatu na soksi.
(ix) Timu yao imepata tuzo.
(x) Rafiki yake amekuja leo.

E. Kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia maneno yaliyo katika kisanduku

Hatua za ufundishaji

(i) Andika ubaoni au kwenye bangokitita maneno yaliyo katika kisanduku kutoka zoezi la 4 E ukurasa wa **43** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma maneno hayo kwa sauti.

KIONGOZI_KISW.indd 43 7/23/21 3:23 PM

(iii) Waongoze wanafunzi kujibu maswali matatu ya mwanzo ya zoezi la 4 E kwa mazungumzo. Hakikisha wanajibu kwa usahihi.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 E lililopo ukurasa wa **43** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) lakini/ingawa/hata hivyo
(ii) ingawa/lakini
(iii) harakaharaka
(iv) walau
(v) hata hivyo/lakini
(vi) wasiwasi
(vii) kwa sababu
(viii) bila
(ix) mithili
(x) kama

F. Kutumia kamusi kueleza maana mbili kwa kila neno na kutunga sentensi moja kwa kila maana ya neno hilo

Hatua za ufundishaji

(i) Andika ubaoni au kwenye bangokitita maneno yaliyopo zoezi la 4 F ukurasa wa **43** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma maneno hayo kwa sauti.

(iii) Waongoze wanafunzi kutumia mifano iliyopo katika Kitabu cha Mwanafunzi ili wapate uelewa wa kufanya zoezi hili.

(iv) Kwa kutumia kamusi, waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 F lililopo ukurasa wa **43** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) mbegu za mpunga mbichi zilizokaangwa na kutwangwa; toa takataka na makapi kwenye nafaka kwa kuzirusharusha ndani ya ungo au kwenye upepo
(ii) si joto si baridi; ushawishi au msukumo wa kufanya jambo
(iii) maadili (heshima); eneo la nyuma au mbele katika jahazi lenye ubao unaotumika kuweka vitu au kukalia
(iv) ondoa kitu chochote kilichovaliwa mwilini; kamata/nasa samaki au kiumbe majini kwa kutumia vifaa maalumu vya uvuvi
(v) muunganiko wa idara nyingi za fani moja; sehemu ya makazi ambayo vitu vingi vinapatikana (sehemu yenye ardhi yenye rutuba ya kutosha)

KIONGOZI_KISW.indd 44 7/23/21 3:23 PM

(vi) ota ukungu kutokana na kuchachuka; toa harufu ya kunuka kutokana na kuoza

(vii) vyuma vilivyolazwa juu ya mataruma ili kufanya njia ya garimoshi kupita; alama au ishara # inayojitokeza kwenye kicharazio au simu

(viii) chombo cha mti, mbao au chuma kinachotumika kupandia au kushukia katika nyumba au nguzo ndefu; daraja analopewa mwajiriwa katika kazi fulani ambalo huonesha kiwango chake cha mshahara

(ix) uwazi uliopo sehemu yoyote ambao unaweza kujazwa au kuwekwa vitu; muda alio nao mtu kwa ajili ya kutekeleza jambo fulani (fursa, wasaa)

(x) maandiko ambayo yananukuliwa katika uandishi wa makala au maandiko mengine; kurudi kutoka safari

G. Kuandika visawe vya maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.

(ii) Toa mifano ya visawe vya maneno kama ilivyooneshwa kwenye Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 G lililopo ukurasa wa **44** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iv) Sahihisha kazi za wanafunzi. Shirikiana na wanafunzi kurekebisha makosa yaliyojitokeza.

Majibu

(i) uvimbe/kisara/nasuri

(ii) ukuu/heshima

(iii) uwazi/utupu/nafasi

(iv) thabiti/imara/madhubuti/kakamavu

(v) kito/jiwe la thamani

(vi) mateso/maonevu/unyonge/taabu

(vii) mazingaombwe/mauzauza

(viii) kosa/lawama/uhalifu/uovu/uasi

(ix) haribu/vuruga/bananga/boronga/vunja

(x) upelelezi/udadisi/upekuzi/ujasusi/utafiti

KIONGOZI_KISW.indd 45 7/23/21 3:23 PM

H. Kupigia mstari neno linaloonesha kauli ya kutendeka

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi ya (i) hadi ya (x) katika zoezi la 4 H lililopo ukurasa wa **44** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waeleze wanafunzi kuwa kauli ya kutendeka huonesha kuwa kitendo kimekamilika au kuwa katika hali timilifu. Kumbuka kuwa kauli ya kutendeka hujidhihirisha katika viambishi tamati **-ek-** na **-ik-**.

(iv) Tumia mifano iliyopo katika zoezi hili kuonesha jinsi ya kupigia mstari neno linaloonesha kauli ya kutendeka.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 H lililopo ukurasa wa **44** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Chakula hiki hakiliki maana hakijaiva vizuri.

(ii) Andika mwandiko unaosomeka kwa urahisi.

(iii) Kiti hiki kimevunjika.

(iv) Chai hii hainyweki maana ni ya moto sana.

(v) Nguo zako nyeupe hazifuliki, labda utumie dawa ya madoa.

(vi) Kunguru hafugiki maana anapenda kuokota majalalani.

(vii) Vitu vimejaa sana uwanjani hata havipangiki.

(viii) Njia hii ni nzuri, inapitika mwaka mzima.

(ix) Kitabu hiki hakisomeki kwani kimechanika vibaya.

(x) Ukumbi umepambika kwa mapambo ya aina mbalimbali.

Somo la 7: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.

(b) Waongoze wanafunzi kujadili matumizi ya methali katika miktadha mbalimbali.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 lililopo ukurasa wa **44** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(d) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, usahihi wa sentensi, mtiririko wa mawazo na matumizi ya methali.

KIONGOZI_KISW.indd 46 7/23/21 3:23 PM

Sura ya Sita

Matumizi ya nahau

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kueleza maana za nahau na kuzitumia katika miktadha mbalimbali. Vilevile, atafanya mazoezi mbalimbali ya lugha na utungaji.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kusoma habari ya **Kijiji cha Mwendokasi**
(b) kueleza maana za nahau
(c) kutumia nahau katika miktadha mbalimbali

Mahitaji: vitu halisi, mazingira halisi, picha (ya kawaida na ya mguso), chati, bangokitita, diski ya igizo (sidii ya igizo), projekta, televisheni, deki, kinyonyi na kompyuta

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kufikiri juu ya matumizi ya nahau katika jamii katika kipengele cha *fikiri* kilichopo ukurasa wa **45** wa Kitabu cha Mwanafunzi.
(b) Waongoze wanafunzi kujadili picha iliyopo ukurasa wa **46** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(c) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari ya **Kijiji cha Mwendokasi** iliyopo ukurasa wa **45 - 47** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.
(d) Waongoze wanafunzi kusimulia kwa maneno machache habari waliyoisoma.
(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **48** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Waongoze kufanya swali la 1- 4 kwa mazungumzo na swali la 5 -10 katika madaftari yao.

KIONGOZI_KISW.indd 47 7/23/21 3:23 PM

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Wakumbushe wanafunzi kanuni na taratibu sahihi za kusoma kwa sauti.

(b) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji sahihi kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi sahihi ya alama za uandishi na kusoma kwa hisia.

(c) Wakati wanafunzi wanasoma, bainisha dosari zinazojitokeza na uzisahihishe.

(d) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo papo hapo.

(e) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha msamiati ufuatao: *hifadhi, mkonga, barazani, tahamaki, wanyamapori, gobore, harakati, maarufu, nyara* na *mzinga* kwa kutumia mbinu ya maelezo, picha na maigizo.

(b) Andika maneno hayo ubaoni; kisha, wanafunzi wasome neno mojamoja na kutamka sauti zinazounda maneno hayo.

(c) Tunga sentensi kwa kutumia maneno hayo; kisha, waulize wanafunzi maana ya neno ulilolitungia sentensi.

Mfano: Watoto wote walitahamaki walipomwona nyoka. Neno tahamaki lina maana gani?

(d) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa kuzungumza. Andika sentensi hizo ubaoni.

(e) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **48** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazotunga hazifanani na zile zilizotolewa mifano.

KIONGOZI_KISW.indd 48 7/23/21 3:23 PM

Somo la 4: Nahau

A. Kueleza maana za nahau

Hatua za ufundishaji

(i) Toa mifano ya nahau na uwaongoze wanafunzi kueleza maana za nahau ulizoandika.

(ii) Waongoze wanafunzi kutaja nahau mbalimbali wanazozifahamu na kueleza maana zake.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 A lililopo ukurasa wa **48** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) kwenda haraka/ongezeka
(ii) haribu mali
(iii) kuwa makini/kosa usingizi
(iv) tembea upesiupesi
(v) funga jela/weka mahabusu
(vi) kosa furaha
(vii) nyamaza
(viii) ondoka/anza safari
(ix) kuwa na hasira
(x) kunywa pombe

B. Kutunga sentensi kwa kutumia nahau

Hatua za ufundishaji

(i) Fundisha nahau zifuatazo: *noa ulimi, kuwa kasuku, roho kwenda juu, kaza kamba, fuja mipango, tega sikio, ota manyoya, kalia kuti kavu, ponda mali* na *ndimi kali* kwa kutumia mbinu ya maelezo, maigizo, oneshombinu na nyinginezo.

(ii) Andika nahau hizo ubaoni; kisha, wanafunzi wazisome kwa sauti.

(iii) Tunga sentensi kwa kutumia nahau; kisha, waulize wanafunzi maana za nahau ulizotungia sentensi.

(iv) Tumia mifano iliyopo katika zoezi la 3 B lililopo ukurasa wa **49** katika Kitabu cha Mwanafunzi kuonesha namna ya kutunga sentensi kwa kutumia nahau.

(v) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia nahau hizo kwa mazungumzo, kisha andika sentensi hizo ubaoni.

(vi) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(vii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 B lililopo ukurasa wa **49** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazotunga hazifanani na zile zilizotolewa mifano.

KIONGOZI_KISW.indd 49 7/23/21 3:23 PM

Somo la 5: Mazoezi ya lugha

A. Kukamilisha sentensi kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye kisanduku

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo jinsi ya kutumia maneno yaliyopo kwenye kisanduku kujaza nafasi zilizo wazi.

(ii) Toa mifano kwa kujaza neno sahihi katika sentensi.

(iii) Tumia mifano iliyopo katika zoezi la 4 A lililopo ukurasa wa **49** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 A lililopo ukurasa wa **49** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) hufunguliwa
(ii) helmeti
(iii) miti
(iv) mazao
(v) matofali
(vi) alama
(vii) shule
(viii) barua
(ix) sikukuu
(x) wimbo

B. Kuandika kwa usahihi maneno yaliyokosewa katika sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo.

(ii) Tumia mifano iliyopo zoezi la 4 B ukurasa wa **50** katika Kitabu cha Mwanafunzi kuwaelekeza wanafunzi jinsi ya kuandika sentensi kwa usahihi kwa kuzingatia ufasaha wa sarufi ya Kiswahili.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 B lililopo ukurasa wa **50** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu

(i) Paka amelala juu ya meza.
(ii) Samaki ni watamu sana kuliko maharage.
(iii) Miti yote iliyokuwa pembezoni mwa barabara imekatwa.
(iv) Ninakuja kwako leo/Nilikuja kwako jana.
(v) Baba amemchapa kaka bakora nyingi.
(vi) Nitakunywa uji wangu kesho asubuhi.

KIONGOZI_KISW.indd 50 7/23/21 3:23 PM

(vii) Shangazi amenunua gari la thamani.
(viii) Wanafunzi wameimba vizuri shairi lao.
(ix) Leo nimenunua pipi kwa shilingi hamsini.
(x) Kitabu changu kina hadithi nzuri.

C. Kuandika kinyume cha maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Tumia mifano iliyopo katika zoezi la 4 C lililopo kwenye ukurasa wa **50** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(ii) Waongoze wanafunzi kutaja vinyume vya maneno yaliyoandikwa ubaoni.
(iii) Andika ubaoni majibu yaliyotajwa na wanafunzi.
(iv) Angalia usahihi wa majibu hayo.
(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 C lililopo ukurasa wa **50** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu

(i) mwembamba
(ii) utulivu/shwari/amani
(iii) kali
(iv) fukia
(v) kamili
(vi) wima
(vii) lazima
(viii) tofautiana
(ix) fumua
(x) dada

D. Kubadili sentensi kuwa katika kauli za kutendwa

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya somo kuwa mabadiliko yatafanyika katika sentensi na kitenzi. Kumbuka kauli ya kutendwa katika kitenzi hutambulishwa na kiambishi **-w-**.
(ii) Tumia mifano iliyopo katika zoezi la 4 D lililopo kwenye ukurasa wa **50** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 D lililopo ukurasa wa **50 - 51** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

KIONGOZI_KISW.indd 51 7/23/21 3:23 PM

Majibu

(i) Maji yanachotwa na Baraka.
(ii) Wali umepikwa na Batuli.
(iii) Vyombo vyote vinaoshwa na kaka.
(iv) Shamba linalimwa na wao.
(v) Mpira unachezwa na watoto.
(vi) Samaki wanavuliwa na wavuvi.
(vii) Koti zuri limevaliwa na mjomba.
(viii) Mihogo mitamu imelimwa na bibi.
(ix) Mayai mengi yanatagwa na kuku.
(x) Nguo nyingi zitafuliwa na Mazoea.

E. Kupigia mstari vitenzi katika sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya somo litakalofundishwa.
(ii) Waeleze wanafunzi kuwa kitenzi huelezea tendo lililofanywa na nomino au kiwakilishi.
(iii) Tumia mifano iliyopo katika zoezi la 4 E lililopo kwenye ukurasa wa **51** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(iv) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi ulizoandika.
(v) Waongoze wanafunzi kutaja vitenzi kwa kila sentensi.
(vi) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 E lililopo ukurasa wa **51** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Bibi <u>anafua</u> nguo na babu <u>anapasua</u> kuni.
(ii) Mwavuli wangu <u>umepotea</u> leo asubuhi.
(iii) Nanasi <u>si</u> tamu.
(iv) Mjuni <u>amemaliza</u> masomo yake ya sekondari.
(v) Mtoto <u>aliogelea</u> mtoni.
(vi) Nahodha <u>anaongoza</u> meli vizuri.
(vii) Mwalimu <u>anafundisha</u> vizuri darasani.
(viii) Daraja <u>limesombwa</u> na maji.
(ix) Shimo <u>limejaa</u> uchafu.
(x) Paka <u>amekunywa</u> maziwa yote.

KIONGOZI_KISW.indd 52 7/23/21 3:23 PM

F. Kujaza fumbo kwa kuzingatia maelekezo

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya somo litakalofundishwa.

(ii) Nakili ubaoni fumbo na maelekezo kama yalivyo katika zoezi la 4 F lililopo ukurasa wa **51** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kujibu fumbo hilo kwa kuandika herufi moja kwenye kila chumba. Tumia herufi kubwa.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 F lililopo ukurasa wa **51** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu

a **d**

A	**D**	**I**	**L**	**I**
N	**J**		**Z**	**L**
D		**I**		**A**
A	**J**		**Z**	**N**
A	**W**	**A**	**L**	**I**

b **c**

G. Kubadili sentensi kuwa katika ukanushi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.

(ii) Tumia mifano iliyopo zoezi la 4 G lililopo ukurasa wa **52** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi zilizopo kwenye zoezi la 4 G lililopo ukurasa wa **52** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 G lililopo ukurasa wa **52** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Babu hajavuna mahindi mengi mwaka huu.

(ii) Bundi si ndege anayefugwa na binadamu.

(iii) Matiku hajapanda basi kuelekea mjini.

(iv) Siku ya Jumamosi hatuendi shuleni.

(v) Baba hapiki chakula jikoni.

KIONGOZI_KISW.indd 53 7/23/21 3:23 PM

(vi) Nyumba yetu haijabomoka.
(vii) Kesho sitapika ugali na dagaa.
(viii) Zakia hasuki nywele za aina mbalimbali
(ix) Bustani ya mboga haijastawi vizuri.
(x) Kaka hajachafua shati la shule.

H. Kuandika visawe vya maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja maneno wanayoyafahamu yenye maana sawa.

(ii) Tumia mifano iliyopo zoezi la 4 H ukurasa wa **52** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano mingine.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 H lililopo ukurasa wa **52** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) mkutano
(ii) ndondi/ngumi/konde
(iii) tunga/kahawa
(iv) uchangamfu/ucheshi
(v) megua
(vi) ghasia
(vii) stoo
(viii) mlio/kelele
(ix) thamani/bei
(x) mzembe/mvivu/mlegevu/legelege

Somo la 6: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo ya somo utakalofundisha.

(b) Waongoze wanafunzi kutaja mambo muhimu ya kuzingatia katika utungaji na yaandike ubaoni.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 lililopo ukurasa wa **52** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(d) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno na herufi kubwa. Zingatia usahihi wa matumizi ya nafsi, nyakati, mnyambuliko wa vitenzi na usahihi wa nahau.

(e) Baada ya kusahihisha, chagua hadithi iliyoandikwa vizuri na wanafunzi waisome darasani kwa sauti.

KIONGOZI_KISW.indd 54 7/23/21 3:23 PM

Sura ya Saba

Aina za maneno

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza aina nane za maneno, ambazo ni nomino (N), kivumishi (V), kitenzi (T), kielezi (E), kiwakilishi (W), kiunganishi (U), kihusishi (H) na kihisishi (Hs). Vilevile, mwanafunzi atapaswa kuainisha aina hizo za maneno zikiwa katika sentensi mbalimbali kwa kutumia vifupisho vya aina hizo.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kusoma masimulizi yanayohusu **Familia ya Mzee Maneno**

(b) kuchambua wahusika katika masimulizi

(c) kutumia aina za maneno katika sentensi

Mahitaji: vitu halisi, picha (ya kawaida na ya mguso), bangokitita na kalamu rashasha

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kufikiri kuhusu aina za maneno zinazotumika katika mazungumzo ya kawaida katika kipengele cha *fikiri* kilichopo ukurasa wa **53** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(b) Waongoze wanafunzi kujadili picha iliyopo ukurasa wa **55** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kusoma kimya masimulizi yaliyopo ukurasa wa **53 - 57** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.

(d) Waongoze wanafunzi kujibu swali hili:
Masimulizi uliyosoma yanahusu nini?

(e) Waongoze wanafunzi kueleza masimulizi waliyosoma yanahusu nini.

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **57** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI_KISW.indd 55 7/23/21 3:23 PM

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu masimulizi ya aina za maneno. Wakumbushe wanafunzi kanuni na taratibu za kusoma masimulizi kwa sauti.

(b) Waongoze wanafunzi kusoma masimulizi kwa kuzingatia kanuni za kusoma kwa sauti. Wanaweza kusoma masimulizi haya zaidi ya mara moja kwa kupokezana.

(c) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzirekebisha.

(d) Waongoze wanafunzi kusoma kwa usahihi. Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(e) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha maana na matumizi ya msamiati ufuatao: *jidai, kinzana, kejeli, pupa, makinika, tenda, viambishi* na *mzizi*.

(b) Andika maneno hayo ubaoni kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya neno mojamoja.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa kuzungumza. Andika sentensi hizo ubaoni.

(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **58** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao. Sentensi ziwe tofauti na zilizotolewa mifano.

Somo la 4: Mazoezi ya lugha

A. Kupigia mstari nomino katika sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Nakili ubaoni sentensi zilizopo katika zoezi la 3 A lililopo ukurasa wa **58** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi mmojammoja kusoma sentensi zote.

(iii) Waongoze wanafunzi kujibu swali la kwanza kama mfano. Rekebisha papo hapo dosari inapojitokeza.

KIONGOZI_KISW.indd 56 7/23/21 3:23 PM

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 A lililopo ukurasa wa **58** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Mayai yamevunjika yote.
(ii) Seremala anatengeneza madawati shuleni.
(iii) Wanafunzi wanatazama mashindano uwanjani.
(iv) Asha hufua nguo zake kila jioni.
(v) Batamzinga anataga mayai bandani.
(vi) Mjomba wangu ameuza gari lake.
(vii) Hii ni kalamu yangu ya risasi.
(viii) Kitabu hiki hakipo mtandaoni.
(ix) Alikaribishwa na Mheshimiwa Diwani wa Kibakwe.
(x) Mwalimu alitufundisha heshima na adabu.

B. Kubadili kauli halisi kuwa kauli taarifa

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya somo litakalofundishwa.
(ii) Nakili sentensi ubaoni au kwenye bangokitita kama zilivyo katika zoezi la 3 B lililopo ukurasa wa **58 - 59** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Toa mfano wa kauli halisi na kauli taarifa.
(iii) Andika sentensi hizo ubaoni na waongoze wanafunzi kubaini alama za mtajo zilizotumika katika kauli halisi.
(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 B lililopo ukurasa wa **58 - 59** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu

(i) Bahati aliuliza kuwa kwa nini magari hayapiti pale siku hizi.
(ii) Madereva walisema kwamba watatii sheria za barabarani.
(iii) Kiranja alimuuliza Lusinde kwa nini alichelewa darasani siku ile.
(iv) Nyambura alisema kwamba alijifunza Kiswahili mwezi uliopita.
(v) Mwanafunzi alisema kuwa kitabu kile ni chake.

KIONGOZI_KISW.indd 57 7/23/21 3:23 PM

(vi) Rozata aliwauliza rafiki zake kwa mshangao kwamba hawaogopi kunyeshewa.

(vii) Mwalimu aliniambia kwamba nikiweke kitabu changu mezani.

(viii) Mtoto alisema kwamba chakula kile kilikuwa ni kitamu.

(ix) Mama alinionya kuwa nilimokuwa ninachezea, mlikuwa na hatari.

(x) Mwalimu aliwaambia wanafunzi kwamba watakwenda Kondoa Irangi kwenye ziara ya kimasomo.

C. Kuandika neno moja linalojumuisha kifungu cha maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi kwa kutumia mifano iliyopo kwenye zoezi la 3 C ukurasa wa **59** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kutaja maneno mbalimbali yaliyopo katika kifungu kinachohusika.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 C ukurasa wa **59** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) viungo
(ii) vyombo
(iii) mavazi/nguo
(iv) udongo
(v) virutubisho
(vi) vinywaji/vinywewa
(vii) silaha
(viii) nishati
(ix) madini
(x) nchi/taifa/dola

D. Kuoanisha maneno ya fungu A na kinyume chake kutoka fungu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye nafasi iliyoachwa wazi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja maneno mbalimbali na vinyume vyake.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 D lililopo kwenye ukurasa wa **59** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI_KISW.indd 58 7/23/21 3:23 PM

Majibu

(i)	*g*	*(vi)*	*f*
(ii)	*j*	*(vii)*	*e*
(iii)	*m*	*(viii)*	*a*
(iv)	*l*	*(ix)*	*b*
(v)	*h*	*(x)*	*c*

E. Kunakili sentensi na kubainisha aina ya neno lililopigiwa mstari kwa kuandika kifupisho cha neno hilo chini yake
Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja aina mbalimbali za maneno. Kumbuka kuna aina nane za maneno na kila aina inasimama kulingana na ilivyotumika.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi kwa kutumia mifano iliyopo zoezi la 3 E lililopo ukurasa wa **60** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 E ukurasa wa **60** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) *Mtoto wake amepotea.*
N

(ii) *Tembo ana masikio makubwa.*
V

(iii) *Wewe unajulikana kila mahali.*
W

(iv) *Nimepokea taarifa muhimu kutoka kwa mkuu wa shule.*
V

(v) *Kumbe! Basi tumejua kwanini haukuja shuleni.*
Hs

(vi) *Mwanafunzi yule ni mtiifu.*
V

(vii) *Hekima ametembea hadi shuleni.*
H

(viii) *Hakunipa chakula wala chai.*
U

KIONGOZI_KISW.indd 59 7/23/21 3:23 PM

(ix) Barua hii imeandikwa na mwanafunzi wa Darasa la Saba.
T

(x) Shukuru alilala fofofo hata hakusikia kelele za kukamatwa
E

kwa mwizi.

F. Kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia fumbo

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya somo litakalofundishwa.

(ii) Waongoze wanafunzi kunakili fumbo kama lilivyochorwa kwenye Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kuunda maneno kwa kutumia fumbo.

(iv) Ongoza wanafunzi kutatua changamoto itakayojitokeza wakati wa kuunda maneno katika fumbo.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 F lililopo ukurasa wa **60** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu

(i)	*rubani*	*(vi)*	*kielezi*
(ii)	*ukwasi*	*(vii)*	*uyoga*
(iii)	*mnajimu*	*(viii)*	*madini*
(iv)	*nomino*	*(ix)*	*katiba*
(v)	*visawe*	*(x)*	*kivumishi*

G. Kupigia mstari viunganishi katika sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja aina mbalimbali za viunganishi. Kumbuka viunganishi vinaunganisha neno na neno au sentensi na sentensi. Viunganishi havina viambishi vya kuambikwa katika neno au katika kupatanishwa kisarufi ndani ya tungo.Viunganishi ni maumbo yasiyobadilika kwa mfano: na, lakini, kwa sababu, ingawa, ila, kwa kuwa, ijapokuwa, pamoja na.

(ii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi mbalimbali zenye viunganishi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 G lililopo ukurasa wa **61** katika Kitabu cha Mwanafunzi

KIONGOZI_KISW.indd 60 7/23/21 3:23 PM

Majibu

(i) Chausiku akitoka shuleni, atapika chakula na kuchota maji.
(ii) Baba, mama, watoto, babu, bibi na shangazi huunda familia.
(iii) Mwanafunzi bora alizawadiwa madaftari pamoja na begi.
(iv) Mwalimu alitoka darasani bila kusema chochote.
(v) Vita dhidi ya umaskini, rushwa na ujinga vinaendelea.
(vi) Masumbuko alijificha kwani hakutaka kuonekana.
(vii) Musa anacheza mpira lakini mimi ninaimba.
(viii) Mwalimu mkuu alihutubia, ijapokuwa mgeni rasmi alikuwapo.
(ix) Muthoni alikwenda Marekani ili kusomea udaktari.
(x) Kibongoto alikwenda nyumbani kwa kuwa hakutaka kuchelewa.

H. Kupigia mstari vielezi katika sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja aina mbalimbali za vielezi. Kumbuka kielezi hutoa taarifa zaidi kuhusu kitenzi, kivumishi au kielezi kingine. Hujibu maswali ya wapi, wakati gani, namna gani tendo lilitendeka na mara ngapi au kwa kiasi gani tendo hujirudia.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi kwa kutumia mifano iliyopo kwenye zoezi la 3 H ukurasa wa **61** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 H lililopo ukurasa wa **61** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu

(i) Mtoto huyo hajaonekana nyumbani tangu alipotoka shuleni.
(ii) Wanafunzi wa Darasa la Saba watakutana kesho.
(iii) Daktari alimwagiza mgonjwa yule anywe dawa mara tatu kwa siku.
(iv) Kibuyu cha bibi kilianguka na kuharibika vibaya.
(v) Fundi seremala alitengeneza kabati kubwa kwa mbao.
(vi) Wahitimu wa Darasa la Saba waliingia ukumbini kwa madaha.

KIONGOZI_KISW.indd 61 7/23/21 3:23 PM

(vii) *Mwizi wa mbuzi alipigwa mara kadhaa kabla ya kuokolewa na polisi.*
(viii) *Bibi kikongwe anatembea polepole.*
(ix) *Wanafunzi wengi hufanya kazi zao harakaharaka.*
(x) *Kiongozi yule huzungumza kiungwana.*

Somo la 5: Methali

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja methali mbalimbali wanazozifahamu.
(b) Tumia mifano ya methali zilizopo ukurasa wa **61** kwenye Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano mingine kwa kuiandika ubaoni; kisha, waongoze wanafunzi wazinakili kwenye madaftari yao.
(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa **61 - 62** kwenye Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

1. *mlipe wema*
2. *asiyefikwa na jeraha*
3. *kaingoje shambani*
4. *hung'aa gizani*
5. *hakimfichi mtu jua*
6. *na moyoni hayupo*
7. *usidhani kapoa*
8. *haikawii kupasuka*
9. *nia mbaya huharibu*
10. *zilimshinda fisi*

Somo la 6: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujadili mambo wanayoyapenda na uyaandike ubaoni.
(b) Toa maelezo kuhusu utungaji wa habari.
(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 lililopo ukurasa wa **62** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwa kuandika kwenye madaftari yao.
(d) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia vitenzi vyote kwenye habari walizozitunga.

KIONGOZI_KISW.indd 62 7/23/21 3:23 PM

Sura ya Nane

Hadithi

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kutunga hadithi fupi, kueleza mafunzo yanayopatikana katika hadithi na kueleza tabia za wahusika.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kusoma hadithi inayohusu **Kijiji cha Fikika**
(b) kueleza tabia ya wahusika katika hadithi
(c) kutunga hadithi kuhusu mazingira yanayomzunguka

Mahitaji: vitabu vya hadithi, chati za maneno, kalamu rashasha, kadi za maneno, kadi za sentensi, picha (ya kawaida na ya mguso), bangokitita na diski (sidii ya matini ya hadithi mbalimbali)

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kufikiri juu ya kazi za mbeba ujumbe wa hadithi katika kipengele cha *fikiri* kilichopo ukurasa wa **63** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya hadithi ya **Kijiji cha Fikika** iliyopo ukurasa wa **63 - 66** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.
(c) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:
    (i) Mzee Bawata aliishi kwa muda gani?
    (ii) Mzee Bawata alipenda nini?
(d) Waongoze wanafunzi kusimulia kwa maneno machache hadithi waliyoisoma.
(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **67** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI_KISW.indd 63 7/23/21 3:23 PM

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo. Eleza unatarajia nini kifanyike katika somo hili.

(b) Soma aya moja au mbili za hadithi kwa kuonesha mfano mzuri wa usomaji kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi ya alama za uandishi na kusoma kwa hisia.

(c) Waongoze wanafunzi kusoma mmojammoja kwa zamu, bila kujali jinsi zao na uwezo wao. Hakikisha wengi wanapata nafasi ya kusoma.

(d) Baini dosari zinazojitokeza wakati wanafunzi wanasoma na uzirekebishe.

(e) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo. Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha msamiati ufuatao: *karne, mzalendo, diriki, minajili, tochi, kichuguu, wazawa, baluni, changanyikiwa, kinyang'anyiro, mzaha, vitukuu* na *vuma*. Andika maneno hayo ubaoni; kisha, wanafunzi wayasome na kueleza maana ya kila neno.

(b) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa kuzungumza. Andika sentensi hizo ubaoni.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **67** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao. Sentensi ziwe tofauti na zilizotolewa mifano wakati wa kujifunza.

(d) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuangalia usahihi wa sentensi.

Somo la 4: Nahau

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja nahau mbalimbali wanazozifahamu.

(b) Andika ubaoni nahau hizo.

(c) Waongoze wanafunzi kueleza maana za nahau hizo.

KIONGOZI_KISW.indd 64 7/23/21 3:23 PM

(d) Waongoze wanafunzi kutaja nahau nyingine zinazoleta taswira hizohizo.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa **68** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

1. *fyatua risasi*
2. *fanya kila njia*
3. *pevuka kwa mtoto wa kike kuingia utu uzimani/kupata hedhi ya kwanza*
4. *nong'oneza*
5. *patwa na maafa au mambo ya huzuni*
6. *waza mambo yasiyowezekana*
7. *vaa vizuri*
8. *fanyia mtu fitina/tafuta njia za kumwangamiza mtu/peleleza mtu*
9. *potea/angamia*
10. *pokea rushwa*

Somo la 5: Mazoezi ya lugha

A. Kukanusha sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kufafanua dhana ya ukanushi kwa kutumia mifano.

(ii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi. Andika sentensi hizo ubaoni; kisha, washirikishe wanafunzi wazikanushe.

(iii) Andika ubaoni majibu ya wanafunzi, kisha washirikishe kurekebisha makosa yanayojitokeza.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 A lililopo ukurasa wa **68** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Mwalimu hafundishi vizuri.

(ii) Mimi sielewi umuhimu wa kunawa mikono kabla na baada ya kula.

(iii) Baraka hapendi kupita njia ile.

(iv) Baba huwa hatumii mitishamba kutibu wagonjwa.

KIONGOZI_KISW.indd 65 7/23/21 3:23 PM

(v) Binamu yangu hana suruali nzuri.
(vi) Ng'ombe wa Juma hatoi maziwa mengi.
(vii) Watoto wa jirani yangu hawana tabia nzuri.
(viii) Mgonjwa hawezi kunywa uji mwenyewe.
(ix) Wanafunzi wengi huwa hawapendi mashindano.
(x) Yule si maarufu kwa mchezo wa ngumi.

B. Kuandika maneno kutokana na silabi zilizochanganywa

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo.
(ii) Changanya silabi za neno; kisha, andika maneno yaliyochanganywa herufi ubaoni.
(iii) Waongoze wanafunzi kuandika maneno hayo kwa usahihi.
(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 B lililopo ukurasa wa **68 - 69** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) mpira
(ii) asasi/siasa
(iii) mtoto
(iv) mwanafunzi
(v) kigogo
(vi) mwalimu
(vii) mwenge
(viii) mfuko
(ix) mkufu
(x) mchele

C. Kuandika visawe vya maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu maneno yenye maana sawa, yaani visawe, kuwa ni maneno tofauti lakini yenye maana sawa.
(ii) Andika ubaoni neno la mfano kutoka katika Kitabu cha Mwanafunzi lililopo katika zoezi la 4 C ukurasa wa **69** bila kisawe chake.
(iii) Waongoze wanafunzi kutaja kisawe cha neno hilo.
(iv) Andika ubaoni kisawe cha neno hilo.
(v) Waongoze wanafunzi kusoma kwa sauti neno na kisawe chake.
(vi) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 C lililopo ukurasa wa **69** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI_KISW.indd 66 7/23/21 3:23 PM

Majibu

(i) *kibwagizo/kipokeo/mkarara*
(ii) *mfundishaji/mfunzi/mkufunzi/msomeshaji/mhadhiri*
(iii) *mazingaombwe/mauzauza/kidanganyamacho/machezo*
(iv) *mwamuzi/msuluhishi/mpatanishi/mtatuzi*
(v) *upesi/wanguwangu*
(vi) *sehemu/mgawo/kasma/rundo*
(vii) *kabichi*
(viii) *vuruga/changanya akili*
(ix) *pungufu/kidogo*
(x) *kisifa*

D. Kuchagua jibu sahihi kwa kulipigia mstari

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo.
(ii) Toa mfano kwa kuandika swali ubaoni ili wanafunzi wachague jibu lililo sahihi kwa kulipigia mstari.
(iii) Waongoze wanafunzi kujadili jinsi ya kujibu swali kwa kutumia mfano uliopo ubaoni.
(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 D lililopo ukurasa wa **69 - 70** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Mwanafunzi anaweza kuandika jibu kwa herufi, neno au yote mawili.

Majibu

(i) *(a) mwashi*
(ii) *(a) kifo*
(iii) *(b) si matusi*
(iv) *(c) binamu*
(v) *(b) kubwa*
(vi) *(c) baa*
(vii) *(c) bisha*
(viii) *(b) mtu mmoja*
(ix) *(d) mate*

KIONGOZI_KISW.indd 67 7/23/21 3:23 PM

Somo la 6: Kazi ya kufanya

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo ya somo.

(b) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 lililopo ukurasa wa **70** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Wasisitize wasimuliwe hadithi na wazazi au walezi wao.

(c) Waongoze wanafunzi kusimulia hadithi walizosimuliwa na wazazi au walezi wao katika kipindi kinachofuata.

(d) Waongoze wanafunzi kueleza mawazo makuu ndani ya hadithi hizo pamoja na tabia za wahusika.

Somo la 7: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo.

(b) Waongoze wanafunzi kutaja mambo muhimu ya kuzingatia katika utungaji wa hadithi na yaandike ubaoni.

(c) Waongoze wanafunzi kujadili mambo waliyoyataja.

(d) Waongoze wanafunzi kurekebisha makosa.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 lililopo ukurasa wa **70** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(f) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, herufi kubwa, mtiririko wa visa na mianzo na miisho ya hadithi.

(g) Baada ya kusahihisha, chagua hadithi iliyoandikwa vizuri na wanafunzi waisome darasani kwa sauti.

KIONGOZI_KISW.indd 68 7/23/21 3:23 PM

Sura ya Tisa

Risala

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi ataendelea kujifunza kuandika risala kwa kuzingatia muundo wake, alama za uandishi pamoja na kueleza matumizi ya risala.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kubaini muundo wa risala
(b) kuandika risala
(c) kueleza matumizi ya risala

Mahitaji: vitu halisi, chati za methali, bangokitita, kalamu rashasha, picha (za kawaida na za mguso) na karatasi ngumu (manila)

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kufikiri juu ya matukio muhimu waliyoshuhudia katika hafla yoyote kwenye kipengele cha *fikiri* katika ukurasa wa **71** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari ya **Kutembelea Bunge** iliyopo ukurasa wa **71 - 74** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.
(c) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:
    (i) Katika kikao cha Bunge, wanafunzi walisikia kitu gani kikijadiliwa?
    (ii) Mwalimu mkuu aliahidi nini baada ya kupokea risala ya wanafunzi wa Darasa la Saba?
(d) Waongoze wanafunzi kusimulia kwa maneno machache habari waliyoisoma.
(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **74** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI_KISW.indd 69 7/23/21 3:23 PM

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo. Eleza unachotarajia kifanyike katika somo hili.

(b) Wakumbushe wanafunzi kuhusu alama za uandishi kwa kuwauliza maswali.

(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi ya alama za uandishi na hisia.

(d) Waongoze wanafunzi kusoma mmojammoja kwa zamu bila kujali jinsi zao na uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma. Bainisha dosari zinazojitokeza wakati wanafunzi wanaposoma na uzirekebishe.

(e) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(f) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha msamiati ufuatao: *mhimili, bunge, hamu, timia, kina, muswada, mheshimiwa, hafla, wasaa, ombi* na *ambatana* kwa kutumia mbinu ya maelekezo, vitu halisi, picha na maigizo.

(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome. Waongoze kueleza maana ya neno mojamoja.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kuzungumza kwa kutumia maneno hayo. Andika sentensi hizo ubaoni.

(d) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **75** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazotunga, hazifanani na zile zilizotolewa kama mifano na zilizotumika kitabuni.

KIONGOZI_KISW.indd 70 7/23/21 3:23 PM

Somo la 4: Miundo

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu namna ya kutumia miundo katika sentensi.
(b) Nakili ubaoni miundo yote iliyopo katika zoezi la 3 ukurasa wa **75 - 76** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(c) Waongoze wanafunzi kusoma miundo hiyo ubaoni.
(d) Waongoze wanafunzi kujadili kanuni za miundo mbalimbali kwa kutumia mifano iliyopo zoezi la 3 ukurasa wa **75 - 76** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(e) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia miundo hiyo kwa mazungumzo na uziandike sentensi hizo ubaoni. Sentensi hizo ziwe tofauti na zile zilizotolewa kwenye mifano.
(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa **75 - 76** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Somo la 5: Nahau

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja nahau wanazozifahamu.
(b) Andika ubaoni nahau zilizotajwa na wanafunzi.
(c) Angalia usahihi wa nahau zilizotajwa na wanafunzi.
(d) Waongoze wanafunzi kueleza maana za nahau walizozitaja.
(e) Tumia mifano kuwaongoza wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa **76** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

1. *dumu kwa kipindi kirefu*
2. *sikiliza kwa makini*
3. *tunza siri*
4. *kuwa makini/kuwa na tahadhari/chukua tahadhari*
5. *ongoza*
6. *kupoteza chanzo au namna ya riziki/poteza kazi*

Tanbihi: Angalia majibu sahihi mengine ya wanafunzi.

KIONGOZI_KISW.indd 71 7/23/21 3:23 PM

Somo la 6: Mazoezi ya Lugha

A. Kupanga sentensi ili kupata kifungu cha habari chenye maana

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi zilizopo zoezi la 5 A ukurasa wa **76 - 77** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waulize wanafunzi kama wamegundua kosa lolote wakati wanasoma sentensi hizo.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 A lililopo ukurasa wa **76 - 77** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Kumbuka kwamba mwanafunzi anaweza kupanga tofauti; hivyo, mtiririko uangaliwe.

Majibu

Msimu wa sikukuu, hasa za mwisho wa mwaka, huwa na shamrashamra za kila aina. Ingawa vitu huuzwa kwa bei ya juu, kila mtu hupenda kununua vitu vipya kwa ajili ya familia yake. Wafanyabiashara hufanya biashara zaidi kipindi hiki. Watoto hufurahi zaidi katika msimu huu. Hufurahia kupata nguo mpya na kwenda kutembea. Wengine husafiri pamoja na wazazi wao kwenda kuwaona ndugu, jamaa na marafiki. Vyombo vya usafiri hupata abiria wengi wanaokwenda na kutoka sehemu mbalimbali. Msimu wa sikukuu ukiisha, waliosafiri hurejea makwao. Pia, wanafunzi hujiandaa kurejea shuleni kwa ajili ya msimu mwingine wa masomo. Wakifika shuleni, kila mmoja husimulia namna alivyofurahia sikukuu za mwisho wa mwaka.

B. Kutumia maneno ili kukamilisha sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma maneno watakayotumia

KIONGOZI_KISW.indd 72 7/23/21 3:23 PM

kujaza nafasi zilizoachwa wazi kabla ya kuanza kufanya zoezi. Maneno hayo yapo juu ya zoezi la 5 B lililopo ukurasa wa **77** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi hilo kwenye madaftari yao.

Majibu

(i) imepiga marufuku
(ii) alishika mkia
(iii) amevaa miwani
(iv) tulipokelewa kwa mikono miwili
(v) alikubali kwa ulimi
(vi) waliangua kicheko
(vii) ilitia fora
(viii) bega kwa bega
(ix) tulipiga pasi

C. Kuoanisha methali kutoka fungu A na maana zake kutoka fungu B

Hatua za ufundishaji

(i) Wagawe wanafunzi katika makundi mawili yenye mchanganyiko wa wavulana na wasichana.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma katika makundi fungu A na fungu B yaliyopo ukurasa wa **78** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Kundi moja wasome methali zilizopo fungu A na kundi lingine wasome maana zake zilizopo fungu B.

(iv) Waongoze wanafunzi kuoanisha methali na maana zake.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 C lililopo ukurasa wa **78** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) d
(ii) f
(iii) a
(iv) h
(v) g
(vi) i
(vii) b
(viii) j
(ix) e
(x) c

KIONGOZI_KISW.indd 73 7/23/21 3:23 PM

D. Kujaza herufi zinazoendana na namba katika jedwali ili kupata maneno sahihi na kutunga sentensi moja kwa kila neno litakalopatikana

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kusoma herufi na namba kama zinavyoonekana katika jedwali.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 D kwa kutumia mfano uliopo kwenye zoezi hili ukurasa wa **78 - 80** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) KATIBU
(ii) SHERIA
(iii) SPIKA
(iv) ZIARA
(v) HAFLA
(vi) WARAKA
(vii) SAFARI
(viii) HOJA
(ix) MJADALA
(x) VIKAO

E. Kuandika sentensi kwa kutumia kinyume cha neno lililokolezwa wino

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.

(ii) Andika ubaoni sentensi mbili za mwanzo za zoezi la 5 E ukurasa wa **80** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi hizo.

(iv) Tumia mfano uliopo katika zoezi hilo kuwaelekeza wanafunzi namna ya kuandika sentensi kwa kutumia neno lililokolezwa wino.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 E lililopo ukurasa wa **80** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

*(i) Wakulima walikwenda shambani wakati wa **mawio**.*
*(ii) Acha **kuniudhi/kunikasirisha** kwa kunivika kilemba cha ukoka.*
*(iii) Yule aliyevaa kilemba ndiye **aliyeshinda**.*
*(iv) **Ungaliwahi** kidogo, ungalipanda basi.*
*(v) Someni habari hii **kwa sauti.***

KIONGOZI_KISW.indd 74 7/23/21 3:23 PM

*(vi) Alianguka kwa kishindo alipokuwa **akipanda** kwenye mnazi.*
*(vii) Gauni hili ni **kubwa** sana kwa binti yangu.*
*(viii) Nani amesema chumvi ni **tamu**?*
*(ix) **Mwisho** wa likizo yako umekaribia.*
*(x) Wageni **wameruhusiwa** kukaa hapa.*

F. Kupanga maneno yanayounda methali yaliyochanganywa ili kupata methali sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja methali wanazozifahamu kwa usahihi.
(ii) Andika methali hizo ubaoni na waongoze wanafunzi kubaini makosa na kuyarekebisha.
(iii) Waongoze wanafunzi kusoma katika vitabu vyao maneno yanayounda methali yaliyochanganywa yaliyopo zoezi la 5 F katika ukurasa wa **80 - 81** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(iv) Waongoze kupanga maneno ili kupata methali sahihi. Toa mfano wa namna ya kufanya zoezi hilo.
(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 F lililopo ukurasa wa **80 - 81** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Kazi ya Mungu haina makosa.
(ii) Usiache mbachao kwa msala upitao.
(iii) Baada ya kisa mkasa.
(iv) Kidole kimoja hakivunji chawa.
(v) Mtegemea cha nduguye hufa maskini.
(vi) Mbio za sakafuni huishia ukingoni.
(vii) Mpanda ovyo hula ovyo.
(viii) Simba mwenda pole ndiye mla nyama.
(ix) Nazi mbovu harabu ya nzima.
(x) Mshindo mkuu huvuma mbali.

KIONGOZI_KISW.indd 75 7/23/21 3:23 PM

G. Kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuchagua jibu sahihi kutoka katika kisanduku

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu utakachofundisha.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma maswali ya zoezi la 5 G lililopo ukurasa wa **81** bila kujaza nafasi zilizoachwa wazi.

(iii) Waeleze kuwa kama sehemu iliyoachwa wazi haijajazwa, sentensi haileti maana.

(iv) Waongoze wanafunzi kujaza swali la kwanza kama mfano.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 G lililopo ukurasa wa **81** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) mnamo
(ii) angekuja
(iii) asingechelewa
(iv) kwa ajili ya
(v) baada ya
(vi) mbali na/baada ya/kabla ya
(vii) kwa muda
(viii) kabla ya
(ix) inakupasa
(x) ngoma

H. Kuandika sentensi katika uhalisia wake

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi ya (i) hadi ya (x), zoezi la 5 H lililopo ukurasa wa **82** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waulize wanafunzi kama wamegundua kosa katika sentensi hizo.

(iv) Tumia mifano iliyopo kwenye zoezi la 5 H (unaweza kuongeza mifano mingine) kuwaelewesha wanafunzi namna ya kufanya zoezi hilo.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 H lililopo ukurasa wa **82** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI_KISW.indd 76 7/23/21 3:23 PM

Majibu

(i) Nahodha anaendesha meli.

(ii) Kazi ya seremala ni kutengeneza samani.

(iii) Kulinda nchi ni jukumu la kila mwananchi.

(iv) Kuongoza magari barabarani ni kazi ya askari wa usalama barabarani.

(v) Wakati wa mafuriko, miundombinu kama vile barabara huharibika.

(vi) Meli hutia nanga bandarini/popote baharini/ziwani/ majini.

(vii) Njia ya garimoshi hutengenezwa kwa vyuma viitwavyo mataruma na reli/Njia ya garimoshi hutengenezwa kwa mataruma na reli.

(viii) Mpira wa miguu huchezwa na wanaume na wanawake.

(ix) Kujenga nyumba ni kazi ya mwashi.

(x) Watoto wote wanatakiwa kupata elimu/Kupata elimu ni haki ya kila mtoto.

Somo la 7: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.

(b) Waongoze wanafunzi kujadili kuhusu muundo na matumizi ya risala katika miktadha mbalimbali.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 lililopo ukurasa wa **82** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(d) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, usahihi wa sentensi na mtiririko wa mawazo.

KIONGOZI_KISW.indd 77 7/23/21 3:23 PM

Sura ya Kumi

Kusoma magazeti

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kusoma kwa kuzingatia maana. Atasoma habari na kutunga sentensi kwa kutumia maneno mapya na kuchanganua mawazo ya msingi katika matini teule za kisiasa, kiuchumi na kijamii kwenye magazeti. Pia, atajifunza msamiati, nahau na miundo. Kisha, atafanya mazoezi mengine ya lugha na utungaji.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kusoma habari ya **Makini asoma makala kwenye gazeti**
(b) kuchanganua mawazo ya msingi katika matini

Mahitaji: vitu halisi, mazingira halisi, picha (ya kawaida na ya mguso), chati, bangokitita, diski ya igizo, sidii ya igizo, projekta, televisheni, deki, kinyonyi na kompyuta

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kufikiri juu ya ujumbe muhimu magazetini kwenye kipengele cha *fikiri* kilichopo ukurasa wa **83** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(b) Waongoze wanafunzi kujadili picha iliyopo katika ukurasa wa **84** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(c) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari ya **Makini asoma makala kwenye gazeti** iliyopo ukurasa wa **83 - 85** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.
(d) Waongoze wanafunzi kusimulia kwa maneno machache habari waliyoisoma.
(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **85** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Maswali 1 - 4 yajibiwe kwa mazungumzo na 5 - 10 kwenye madaftari yao.

KIONGOZI_KISW.indd 78 7/23/21 3:23 PM

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Wakumbushe wanafunzi kanuni na taratibu sahihi za kusoma kwa sauti.

(b) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji sahihi kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi sahihi ya alama za uandishi na kusoma kwa hisia.

(c) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na uzisahihishe.

(d) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo papo hapo.

(e) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha msamiati ufuatao: *makala, uchongaji, ufinyanzi, umakanika, ufumaji, hitimu, nadharia, kozi, nidhamu* na *shauri* kwa kutumia mbinu ya maelezo, picha na maigizo.

(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha waongoze wanafunzi wasome neno mojamoja.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa kuzungumza. Andika sentensi hizo ubaoni.

(d) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **86** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazotunga hazifanani na zile zilizotolewa katika mifano.

Somo la 4: Miundo

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu namna ya kutumia miundo katika sentensi.

(b) Nakili ubaoni au kwenye bangokitita miundo yote iliyopo katika zoezi la 3 ukurasa wa **86** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI_KISW.indd 79 7/23/21 3:23 PM

(c) Waongoze wanafunzi kusoma miundo hiyo.
(d) Tumia mifano ya sentensi zenye miundo iliyopo katika zoezi la 3 ukurasa wa **86** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(e) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia miundo hiyo kwa mazungumzo na andika sentensi hizo ubaoni.
(f) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.
(g) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa **86** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Sentensi hizo ziwe tofauti na zile zilizotolewa kwenye mifano.

Somo la 5: Nahau na misemo

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa.
(b) Waongoze wanafunzi kutaja nahau mbalimbali wanazozifahamu na kueleza maana zake.
(c) Toa mifano ya nahau na uwaongoze wanafunzi kueleza maana za nahau ulizoandika.
(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa **86** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

1. *zingatia*
2. *fika mwisho wa jambo*
3. *kwa pamoja/kwa kufuatana*
4. *kuwa na kiburi*
5. *tawala mtu, pumbaza*
6. *fanya kitu kiwe bora/boresha*
7. *kuwa na wivu*
8. *hali ya kusita*
9. *asiye na haya au aibu*
10. *andaa chakula mezani*

Somo la 6: Mazoezi ya lugha

A. Kuandika umoja au wingi wa maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa.
(ii) Waongoze wanafunzi kuandika umoja au wingi wa maneno kwa kutumia mifano ya zoezi la 5 A lililopo ukurasa wa **87** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI_KISW.indd 80 7/23/21 3:23 PM

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 A lililopo ukurasa wa **87** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) mizigo
(ii) mtafiti
(iii) abiria
(iv) wanamuziki
(v) washindi
(vi) mpole
(vii) pera
(viii) nywele
(ix) mpira
(x) mikoba

B. Kuandika vinyume vya maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa.
(ii) Andika ubaoni maneno machache bila vinyume vyake.
(iii) Tumia mifano iliyopo katika zoezi la 5 B ukurasa **87** katika Kitabu cha Mwanafunzi kuwaelezea dhana ya kinyume. Unaweza kuongeza mifano mingine.
(iv) Waongoze wanafunzi kutaja vinyume vya maneno yaliyoandikwa ubaoni.
(v) Andika ubaoni majibu yaliyotajwa na wanafunzi.
(vi) Angalia usahihi wa majibu hayo.
(vii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 B lililopo ukurasa wa **87** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu

(i) kufeli/kushindwa
(ii) kiume
(iii) shangazi
(iv) mlegevu/goigoi
(v) jumla
(vi) fichua
(vii) vuta
(viii) noti
(ix) nyeupe
(x) Magharibi

KIONGOZI_KISW.indd 81 7/23/21 3:23 PM

C. Kubadili sentensi kuwa katika hali timilifu

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa.

(ii) Waongoze wanafunzi kutaja nyakati mbalimbali.

(iii) Tumia mifano iliyopo katika zoezi la 5 C lililopo ukurasa wa **88** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano mingine.

(iv) Waongoze wanafunzi kubadili sentensi kuwa katika hali timilifu. Kumbuka kuwa kiambishi kinachoonesha hali timilifu katika kitenzi ni **-me-**.

(v) Andika ubaoni sentensi zilizopo ukurasa wa **88** katika Kitabu cha cha Mwanafunzi.

(vi) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi zilizoandikwa ubaoni.

(vii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 C lililopo ukurasa wa **88** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Mama amepika chakula kingi.

(ii) Wanafunzi wa Darasa la Saba wameotesha mahindi shambani.

(iii) Ng'ombe amechinjwa leo jioni.

(iv) Dada yangu amefaulu mitihani yake.

(v) Mwalimu ameingia darasani kimyakimya.

(vi) Mto umefurika wakati wa mvua.

(vii) Bibi amepasua kuni.

(viii) Busara ametoka kutibiwa hospitalini.

(ix) Magoti amehudhuria kikao cha wazazi.

(x) Shamba lote limepandwa vizuri.

D. Kanusha sentensi zifuatazo

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo unalotaka kufundisha.

(ii) Tumia mifano iliyopo katika zoezi la 5 D lililopo ukurasa **88** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano mingine.

KIONGOZI_KISW.indd 82 7/23/21 3:23 PM

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 D lililopo ukurasa wa **88** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Juma hajashinda mashindano ya riadha.
(ii) Hatufundishwi somo la Kiingereza kila siku shuleni.
(iii) Mariamu hatanunua kitabu kizuri.
(iv) Kaka yangu havui samaki bwawani.
(v) Sijawaona wanyama wengi mbugani.
(vi) Mzava hakufua shati lake.
(vii) Shangazi hali senene kwa wingi.
(viii) Hajauza viatu vyake vya shule.
(ix) Kizota hafugi kuku na mbuzi.
(x) Meli haijazama ziwani.

E. Kuandika neno tofauti na mengine

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa.
(ii) Tumia mifano iliyopo zoezi la 5 E ukurasa wa **89** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano mingine.
(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 E lililopo ukurasa wa **89** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) meza
(ii) sufuria
(iii) raba
(iv) nyama
(v) buibui
(vi) mwanafunzi
(vii) bati
(viii) mchicha
(ix) mikono
(x) karatasi

F. Kupanga herufi ili kupata maneno yenye maana

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja maneno na uyaandike ubaoni. Changanya herufi za maneno hayo na uziandike ubaoni.
(ii) Shirikisha wanafunzi kupangilia herufi za maneno hayo ili kuleta neno sahihi na uliandike ubaoni.

KIONGOZI_KISW.indd 83 7/23/21 3:23 PM

(iii) Tumia mifano iliyopo katika zoezi la 5 F lililopo ukurasa wa **89** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano mingine.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 F lililopo ukurasa wa **89** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) kielezi
(ii) mpishi/mshipi
(iii) ugua
(iv) mwalimu
(v) potea/topea
(vi) gauni/gunia
(vii) dagaa
(viii) polisi
(ix) limau
(x) hodari

G. Kunominisha vitenzi

Hatua za ufundishaji

(i) Andika ubaoni maneno machache bila nomino zake.

(ii) Tumia mifano iliyopo katika zoezi la 5 G lililopo ukurasa wa **89** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano mingine.

(iii) Waongoze wanafunzi kutaja nomino za vitendo viliyoandikwa ubaoni.

(iv) Andika ubaoni majibu yaliyotajwa na wanafunzi.

(v) Angalia usahihi wa majibu hayo.

(vi) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 G lililopo ukurasa wa **89 - 90** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu

(i) mpambaji/pambo/upambaji/mpambe
(ii) mchezaji/uchezaji/mchezo
(iii) mkataji/ukataji/mkato
(iv) mfuaji/ufuaji/mfuo
(v) mpimaji/upimaji/kipimo/kipimio
(vi) muuzaji/uuzaji/mauzo
(vii) mwimbaji/uimbaji/wimbo
(viii) mchungaji/uchungaji/chungio/kichungi
(ix) mwindaji/uwindaji/windo
(x) mvutaji/uvutaji/kivutio/mvuto/mvutano

KIONGOZI_KISW.indd 84 7/23/21 3:23 PM

Tanbihi: Haya ni baadhi ya majibu. Unaweza kuongeza majibu mengine yaliyo sahihi.

Somo la 7: Kazi ya kufanya

Hatua za ufundishaji

(a) Waeleze wanafunzi lengo la kusoma magazeti.

(b) Wafahamishe kuwa lengo ni kubaini maneno mapya, kueleza maana za maneno hayo na kuyatungia sentensi.

(c) Waongoze wanafunzi kuchagua gazeti moja; kisha, waongoze jinsi ya kusoma kwa kuzingatia malengo ya usomaji. Wasisitize wanafunzi kuchagua magazeti yenye maadili na si ya udaku.

(d) Waongoze wanafunzi kubaini katika gazeti maneno mapya, yaani maneno ambayo maana zake hawazifahamu na kueleza maana zake; kisha, watunge sentensi kwa kutumia maneno hayo.

(e) Pitia kazi za wanafunzi na kuzisahihisha.

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 lililopo ukurasa wa **90** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Somo la 8: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo ya somo.

(b) Waongoze wanafunzi kutaja mambo muhimu ya kuzingatia katika utungaji na uyaandike ubaoni.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 7 lililopo ukurasa wa **90** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(d) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno na herufi kubwa. Zingatia usahihi wa matumizi ya nafsi, nyakati na mnyambuliko wa vitenzi.

(e) Chagua hadithi iliyoandikwa vizuri (yenye mtiririko mzuri wa mawazo na matumizi sahihi ya alama za uandishi) na wanafunzi waisome darasani kwa sauti.

KIONGOZI_KISW.indd 85 7/23/21 3:23 PM

Sura ya Kumi na Moja

Barua ya kirafiki na rasmi

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza muundo wa barua ya kirafiki na rasmi, kuandika barua hizo na kueleza matumizi yake. Vilevile, atajifunza namna ya kuzituma.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kueleza muundo wa barua ya kirafiki na rasmi
(b) kuandika barua ya kirafiki na rasmi
(c) kueleza matumizi ya barua za kirafiki na rasmi
(d) kutuma barua

Mahitaji: vitu halisi (bahasha, kalamu, karatasi, stempu, rangi, gundi na mkasi)

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kufikiri juu ya sifa za barua za kirafiki na rasmi katika kipengele cha *fikiri* kilichopo ukurasa wa **91** kwenye Kitabu cha Mwanafunzi.
(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari ya **Kijiji cha Katale** iliyopo ukurasa **91 - 94** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.
(c) Waongoze wanafunzi kujibu swali hili:
Taja majina ya wahusika waliotajwa katika habari.
(d) Waongoze wanafunzi wasimulie kwa maneno machache habari waliyoisoma.
(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **95** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI_KISW.indd 86 7/23/21 3:23 PM

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo. Eleza unachotarajia kifanyike katika somo hili.

(b) Wakumbushe wanafunzi alama za uandishi kwa kuwauliza maswali.

(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi ya alama za uandishi, na kusoma kwa hisia.

(d) Waongoze wanafunzi kusoma mmojammoja kwa zamu bila kujali jinsi zao na uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi iwezekanavyo wanapata nafasi ya kusoma.

(e) Baini dosari zinazojitokeza wakati wanafunzi wanasoma na uzirekebishe.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha msamiati ufuatao: *tetemeko, barua, bahasha, stempu, posta, miundombinu, hatima, changia, kaya* na *kamilika* kwa kutumia mbinu ya maelezo, vitu halisi, picha, maigizo na mbinu nyinginezo.

(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome.

(c) Waongoze wanafunzi kueleza maana ya neno mojamoja.

(d) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kuzungumza kwa kutumia maneno hayo. Andika sentensi hizo ubaoni.

(e) Kagua usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **95** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazotunga si zile zilizotumika kwenye mifano.

KIONGOZI_KISW.indd 87 7/23/21 3:23 PM

Somo la 4: Mazoezi ya lugha

A. Kuchagua neno sahihi kutoka kwenye mabano na kujaza nafasi zilizoachwa wazi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya somo litakalofundishwa.

(ii) Toa mifano ya kuchagua neno sahihi kutoka kwenye mabano na kujaza katika nafasi zilizoachwa wazi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 A lililopo ukurasa wa **95 - 96** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) limeungua
(ii) kurahisisha
(iii) walishirikiana
(iv) amelazwa
(v) madhara
(vi) umaskini
(vii) ambaye
(viii) yao
(ix) ule
(x) aliyoyasema

B. Kuandika KWELI au SI KWELI

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kwa kutoa mfano wa sentensi za kujibu KWELI au SI KWELI. Unaweza kutumia sentensi ya kwanza au ya pili kama mfano katika zoezi la 3 B lililopo ukurasa wa **96** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Ongeza sentensi nyingine ili kujenga umahiri katika zoezi hili.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 B lililopo ukurasa wa **96** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) SI KWELI
(ii) SI KWELI
(iii) KWELI
(iv) KWELI
(v) SI KWELI
(vi) KWELI
(vii) SI KWELI
(viii) KWELI
(ix) SI KWELI
(x) KWELI

KIONGOZI_KISW.indd 88 7/23/21 3:23 PM

C. Kuandika sentensi katika wingi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu umoja na wingi.

(ii) Tumia mifano iliyopo zoezi la 3 C ukurasa wa **96** katika Kitabu cha Mwanafunzi kujadili dhana ya umoja na wingi. Unaweza kuongeza mifano mingine.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 C lililopo ukurasa **96 - 97** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Shule zetu zimefungwa; hivyo, hatutakwenda shuleni.

(ii) Vitabu vyetu vimechanika; tumeshindwa kufanya kazi zetu za nyumbani.

(iii) Wanafunzi wa Darasa la Saba wamefaulu mitihani yao vizuri.

(iv) Tunajifunza lugha zetu ili tuwe mahiri katika mawasiliano.

(v) Vijana wanajua kusoma na kuandika vizuri.

(vi) Watoto watiifu na wenye adabu hupendwa na wazazi wao.

(vii) Yatupasa kusoma kwa bidii ili kufaulu mitihani yetu.

(viii) Wanakijiji hao walikuwa wakulima na wafugaji.

(ix) Mabwanashamba waliwaeleza wanafunzi jinsi ya kulima mbogamboga.

(x) Wanafunzi waliotoa hoja madarasani walipongezwa kwa kupewa zawadi.

D. Kupanga herufi zilizochanganywa ili kuunda neno sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Andika maneno yaliyochanganywa herufi ubaoni.

(ii) Waongoze wanafunzi kupanga herufi ili kupata neno au maneno sahihi.

(iii) Wape nafasi wanafunzi wajaribu kadiri inavyowezekana.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 D lililopo ukurasa wa **97** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI_KISW.indd 89 7/23/21 3:23 PM

Majibu

(i) familia
(ii) hekima/kihema
(iii) kitabu/katibu/tibuka/kabuti
(iv) kalenda
(v) kiganja
(vi) muuguzi
(vii) mnyama
(viii) msaada
(ix) barua/aruba/rubaa
(x) bidhaa/baadhi

E. Kubadili sentensi ziwe katika wakati ujao

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kusoma kwa usahihi sentensi zilizopo kwenye vitabu vyao.

(ii) Waongoze wanafunzi kutaja nyakati kwa kila sentensi wanayoisoma.

(iii) Waongoze wanafunzi kutambua viambishi vinavyotumika katika wakati uliopo na ujao, yaani "**-na-**" na "**-ta-**."

(iv) Wanafunzi wanaposoma na kutaja aina ya wakati uliotumiwa katika sentensi, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha papo hapo. Kumbuka kuwa viambishi vinavyoonesha nyakati katika kitenzi ni '**-na-**' (wakati uliopo) na '**-ta-**' (wakati ujao).

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 E lililopo ukurasa wa **97**, katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Vyakula aina ya wanga vitasaidia kujenga mwili.
(ii) Mwalimu Mkumbukwa atatufundisha habari za mashujaa.
(iii) Serikali itachukua hatua katika kulinda rasilimali za taifa.
(iv) Gari litakalopita kijijini kwao litakwenda Kilwa.
(v) Wanafunzi watakwenda kumwona mwenzao.
(vi) Fikiri atasifiwa sana kwa hekima na juhudi katika mafunzo ya shuleni na nyumbani.
(vii) Tutakumbuka Sikukuu ya Mashujaa.
(viii) Lusato atazungumza lugha ya Kiswahili kwa ufasaha.
(ix) Chivuma atasimama chini ya mchungwa akiwasubiri wenzake.
(x) Mtoto atalifunga dirisha litakaloingiza hewa.

KIONGOZI_KISW.indd 90 7/23/21 3:23 PM

F. Kukanusha sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kufafanua dhana ya ukanushi.

(ii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi zilizo katika uyakinishi. Andika sentensi hizo ubaoni, kisha waongoze kuzikanusha. Andika ubaoni majibu ya wanafunzi, kisha washirikishe kurekebisha makosa.

(iii) Wape wanafunzi mazoezi mengi ya ukanushi kadiri inavyowezekana.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 F lililopo ukurasa wa **98** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Mzee Mbagala na jamaa yake hawana dhiki ya chakula.

(ii) Mashine yetu haisagi magunia themanini ya mahindi kwa siku.

(iii) Mtangazaji hatangazi kwa kipazasauti.

(iv) Mwenyekiti hakufafanua bajeti ya kijiji.

(v) Ndizi zile zisingekuwa mbivu, zisingedondoka zenyewe.

(vi) Mashindano ya nyimbo hayakufanyika ndani ya jumba la makumbusho.

(vii) Sadiki hakuwa mwanafunzi mwenye bidii darasani.

(viii) Maziwa ya mtoto hayajamwagika.

(ix) Sitanunua viatu bei isiposhuka.

(x) Shangazi hajapika chakula cha wageni.

G. Kuandika visawe na vinyume vya maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutoa maana ya visawe na vinyume kwa kutoa mifano mbalimbali.

(ii) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 3 G ukurasa wa **98** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 G lililopo ukurasa wa **98** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI_KISW.indd 91 7/23/21 3:23 PM

Majibu

Na.	Neno	Kisawe	Kinyume
(i)	*zorota*	*legalega/tepetea/tepeta*	*imarika*
(ii)	*kwanza*	*awali/mwanzo/chanzo*	*mwisho/kaditama/kikomo/ tamati*
(iii)	*lingana*	*fanana/shabihiana/wiana*	*tofautiana/hitilafiana/kinzana*
(iv)	*adimu*	*nadra/chache/haba*	*tele/-ingi*
(v)	*ugumu*	*ukavu/uyabisi/ukame*	*wepesi/urahisi/ulaini/uoevu*
(vi)	*uwanda*	*tambarare*	*mlima/mwinuko*
(vii)	*legevu*	*tepetevu/goigoi/zembe*	*shupavu/imara/madhubuti*
(viii)	*amani*	*salama/utulivu/shwari*	*fujo/ghasia/ugomvi/vita/vurugu*
(ix)	*adabu*	*heshima/nidhamu/staha/ utiifu*	*dharau/kiburi*
(x)	*omboleza*	*sikitika/huzunika*	*furahia/sherehekea*

H. Kupigia mstari neno lililo tofauti na maneno mengine

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya somo utakalofundisha.

(ii) Toa mifano michache kwa kupigia mstari neno ambalo ni tofauti na mengine.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 H lililopo ukurasa wa **98 - 99** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) kashifu
(ii) chukia
(iii) jongoo
(iv) mfuasi
(v) nyamaza
(vi) lia
(vii) uvivu
(viii) tabasamu
(ix) unga
(x) ng'atuka

KIONGOZI_KISW.indd 92 7/23/21 3:23 PM

Somo la 5: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.

(b) Ongoza majadiliano kuhusu muundo wa barua rasmi na barua ya kirafiki.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 A na B lililopo ukurasa wa **99 - 100** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwa kuzingatia tofauti za miundo ya barua hizo.

(d) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno na usahihi wa sentensi.

Majibu: Zoezi la 4 A

1. *Kikombo*
2. *Mpwapwa*
3. *12/02/2020*
4. *Dodoma*
5. *Husika na somo lililotajwa hapo juu*
6. *Kikombo*
7. *Spika*
8. *kujifunza shughuli mbalimbali*
9. *Wanafunzi wa Darasa la Saba*

Somo la 6: Kazi ya kufanya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 lililopo ukurasa wa **100** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(b) Waongoze wanafunzi kutaja matumizi ya bahasha.

(c) Waongoze wanafunzi kuchagua sura ya bahasha wanayotaka kuitengeneza.

(d) Waongoze kuifumua bahasha hiyo; kisha, wailaze juu ya karatasi ngumu yenye ukubwa zaidi ya bahasha hiyo.

(e) Waongoze wachore ramani ya bahasha hiyo kwa kufuatisha;

KIONGOZI_KISW.indd 93 7/23/21 3:23 PM

kisha, wakate kigezo cha bahasha cha karatasi ngumu.

(f) Waongoze kutumia kigezo hicho kuchorea sura za bahasha kwenye karatasi walizoziandaa.

(g) Waongoze wakate sura hizo za bahasha; kisha, wachore mistari hafifu ya penseli kuonesha sehemu zitakazokunjwa.

(h) Waongoze kukunja ramani hiyo ya bahasha kwa kukunja masikio yote manne kuelekea upande wa ndani, wapake gundi na waunganishe sehemu hizo, kisha waweke bahasha mahali safi kivulini ili gundi ikauke.

(i) Waongoze wanafunzi kuweka barua zao ndani ya bahasha, kisha wabandike stempu na kuandika anwani sahihi ya mwandikiwa.

(j) Waongoze wanafunzi kupeleka barua zao posta iliyo karibu. Kama hakuna ofisi ya posta karibu, tengeneza mfano wa mahali pa kutumbukizia barua ili wanafunzi watumbukize barua zao.

KIONGOZI_KISW.indd 94 7/23/21 3:23 PM

Sura ya Kumi na Mbili

Kadi za mialiko

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza muundo wa kadi za mialiko na mambo ya kuzingatia wakati wa kuandika kadi za mialiko. Vilevile, ataeleza matumizi ya kadi za mialiko katika maisha ya kila siku.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kusoma hadithi
(b) kueleza maana ya kadi za mialiko
(c) kueleza muundo wa kadi za mialiko
(d) kueleza matumizi ya kadi za mialiko
(e) kuandaa kadi za mialiko

Mahitaji: kadi mbalimbali za mialiko, manila na kalamu rashasha

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kufikiri namna walivyopata taarifa ya kuhudhuria sherehe yoyote katika kipengele cha *fikiri* kilichopo ukurasa wa **101** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(b) Waongoze wanafunzi kujadili picha iliyopo ukurasa wa **103** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(c) Waongoze wanafunzi kusoma kimya hadithi iliyopo ukurasa wa **101 - 104** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Wasome bila kufuatisha vidole wala kutoa sauti.
(d) Waulize wanafunzi maswali yafuatayo:
    (i) Je, umewahi kuhudhuria sherehe yoyote?
    (ii) Ulialikwa?
    (iii) Kama hukualikwa uliwezaje kuhudhuria sherehe hiyo?
    (iv) Ulihudumiwaje?
(e) Waongoze wanafunzi kusimulia kwa maneno machache hadithi waliyoisoma.
(f) Waongoze wanafunzi kujadili kuhusu lugha ya picha (taswira) iliyotumika katika hadithi hii.
(g) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **104** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI_KISW.indd 95 7/23/21 3:23 PM

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo.

(b) Wakumbushe wanafunzi alama za uandishi kwa kuuliza maswali.

(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji sahihi kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi sahihi ya alama za uandishi na kusoma kwa hisia.

(d) Waongoze wanafunzi mmojammoja kusoma kwa zamu, bila kujali jinsi zao na uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma kadiri muda utakavyoruhusu.

(e) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha msamiati ufuatao: *chochea, kabambe, kamati, bundi, nono, marula, kadi, mwaliko, wadhifa* na *timilifu* kwa kutumia mbinu ya vitu halisi, maelezo, picha na maigizo. Kumbuka maana ya neno marula ni matundapori ya rangi ya manjano yanayopendwa na wanyamapori kama tembo.

(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya neno mojamoja kama lilivyotumika kwenye habari.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa mazungumzo kwa kutumia maneno hayo. Andika sentensi hizo ubaoni na kuangalia kama ziko sahihi. Washirikishe wanafunzi wazisome kwa sauti.

(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **104** katika Kitabu cha Mwanafunzi.Wasisitize kuwa sentensi watakazozitunga zisifanane na zile walizozitunga katika mifano darasani.

KIONGOZI_KISW.indd 96 7/23/21 3:23 PM

Somo la 4: Mazoezi ya lugha

A. Kuandika umoja wa sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa.

(ii) Waongoze wanafunzi kuandika maneno yanayoonesha umoja.

(iii) Chopeka neno lililo kwenye umoja kwenye orodha ya maneno yaliyo katika wingi. Ongoza wanafunzi kubaini neno linaloonesha umoja. Pia, tumia mfano uliopo kwenye zoezi la 3 A lililopo ukurasa wa **104** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 A lililopo ukurasa wa **104 - 105** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Mnyama alihudhuria sherehe ya kumaliza mwaka.

(ii) Mwanakamati alifanya kazi kwa bidii.

(iii) Popo haoni vizuri mchana.

(iv) Mimi nilipokea kadi ya mwaliko wa mahafali.

(v) Mwalikwa alifurahishwa na maandalizi ya sherehe.

(vi) Alilipuka kwa furaha baada ya kula tunda la marula.

(vii) Mwanafunzi anasoma kwa bidii ili afanye vizuri katika mtihani wake.

(viii) Kadi ya mwaliko ndiyo inayompa mtu idhini ya kuhudhuria kwenye sherehe.

(ix) Kinywaji kilimtosha mgeni.

(x) Popo aliandaa kadi kwa rangi ya kuvutia.

B. Kuandika KWELI au SI KWELI kwenye sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa.

(ii) Waongoze wanafunzi kujadiliana jinsi ya kujibu maswali ya kweli au si kweli.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 B lililopo ukurasa wa **105** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

KIONGOZI_KISW.indd 97 7/23/21 3:23 PM

Majibu

(i) *KWELI*
(ii) *SI KWELI*
(iii) *KWELI*
(iv) *SI KWELI*
(v) *KWELI*
(vi) *KWELI*
(vii) *SI KWELI*
(viii) *SI KWELI*
(ix) *SI KWELI*
(x) *KWELI*

C. Kuandika visawe vya maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa.
(ii) Waongoze wanafunzi kusoma maneno yaliyopo zoezi la 3 C lililopo ukurasa wa **105** kwenye Kitabu cha Mwanafunzi.
(iii) Waongoze wanafunzi kutaja visawe vya maneno hayo kwa mazungumzo.
(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 C lililopo ukurasa wa **105** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu

(i) *tarizi*
(ii) *ukaribisho/mwito/jaliko*
(iii) *tamasha/shangwe/tafrija/karamu/maadhimisho/dhifa/shamrashamra/hafla*
(iv) *kinywewa*
(v) *maakuli/mlo*
(vi) *nzima/zima/timilifu/timamu*
(vii) *furahi*
(viii) *sheria/utaratibu/taratibu*

D. Kukamilisha fumbo kwa kutumia maelezo ya kwenda chini na kwenda kulia

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya somo litakalofundishwa.
(ii) Nakili fumbo na maelekezo ya kwenda chini na kulia ubaoni au kwenye bangokitita kama yalivyo katika zoezi la 3 D lililopo ukurasa wa **106** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI_KISW.indd 98 7/23/21 3:23 PM

(iii) Waongoze wanafunzi kujibu fumbo hilo kwa kutumia mfano wa kwenda chini wa swali la kwanza kwa kuuliza swali hili:

1. *Mtu aliyetembelea mahali fulani kwa mara ya kwanza anaitwaje? (Herufi 5) - MGENI*

(iv) Andika jibu hilo kwenye vyumba vya kuanzia namba 1 kwenda chini. Kila chumba kiandikwe herufi moja tu. Tumia herufi kubwa.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 D lililopo ukurasa wa **106** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu

[1]M	**W**	**[2]A**	**L**	**I**	**[3]K**	**O**	
G		**L**			**I**		
E		**I**			**T**		
N		**K**		**[4]K**	**A**	**D**	**I**
I		**A**			**M**		
					B		
[5]S	**H**	**[6]U**	**G**	**H**	**U**	**L**	**I**
		L			**L**		
		I			**I**		
		P			**S**		
[7]S	**H**	**E**	**R**	**E**	**H**	**E**	
					O		

E. Kukamilisha jedwali kwa kubainisha idadi ya silabi, konsonanti na irabu katika maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa.

(ii) Nakili jedwali lililopo kwenye zoezi la 3 E ukurasa wa **107** ubaoni na uwaongoze wanafunzi kwa kutumia mfano kubaini konsonanti na irabu za maneno hayo. Mwanafunzi ahesabu kila silabi, irabu na konsonanti, hata kama zinajirudiarudia katika neno.

KIONGOZI_KISW.indd 99 7/23/21 3:23 PM

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 E ukurasa wa **107** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

Na.	*Neno*	*Silabi*	*Konsonanti*	*Irabu*
(i)	*themanini*	*4*	*5*	*4*
(ii)	*zambarau*	*4*	*4*	*4*
(iii)	*nta*	*2*	*2*	*1*
(iv)	*waliotukimbilia*	*8*	*7*	*8*
(v)	*chuchumaa*	*4*	*3*	*4*
(vi)	*aghalabu*	*4*	*4*	*4*
(vii)	*sisimizi*	*4*	*4*	*4*
(viii)	*konsonanti*	*4*	*6*	*4*
(ix)	*mzalendo*	*4*	*5*	*3*
(x)	*blanketi*	*3*	*5*	*3*

Somo la 5: Kazi ya kufanya

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa.

(b) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa **107** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kukusanya kadi za mwaliko za matukio mbalimbali.

(d) Waongoze wanafunzi kujadili muundo wa kadi hizo na matumizi yake.

KIONGOZI_KISW.indd 100 7/23/21 3:23 PM

Somo la 6: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa.

(b) Waongoze wanafunzi kutaja mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa kadi za mwaliko ambayo ni jina la mwandishi na anwani yake, nyadhifa za waalikwa, tarehe ya sherehe, lengo la sherehe, mahali sherehe itakapofanyika, muda wa kuanza na kumaliza sherehe na mawasiliano.

(c) Waongoze wanafunzi kujadili mambo waliyoyataja.

(d) Rekebisha makosa yaliyojitokeza, kisha waruhusu wanafunzi kuandika kadi za mialiko.

(e) Gawa karatasi ngumu na rangi kwa kila mwanafunzi. Pia, unaweza kuwashirikisha wanafunzi kuleta karatasi hizo.

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 lililopo ukurasa wa **107** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(g) Sahihisha kazi kwa kuzingatia mambo muhimu yanayohitajika katika kadi za mialiko.

KIONGOZI_KISW.indd 101 7/23/21 3:23 PM

Sura ya Kumi na Tatu

Insha

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza muundo wa insha na kuandika insha kuhusu uharibifu wa mazingira kwa kuzingatia alama za uandishi.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kubaini muundo wa insha
(b) kuandika insha kuhusu uharibifu wa mazingira

Mahitaji: insha za mfano, manila na kalamu rashasha

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo.
(b) Waongoze wanafunzi kufikiri juu ya sifa za insha wanazozifahamu katika kipengele cha *fikiri* kilichopo ukurasa wa **108** wa Kitabu cha Mwanafunzi.
(c) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari ya **Uharibifu wa mazingira** iliyopo ukurasa wa **108 - 110** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.
(d) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:
    (i) Kitu gani kilimfanya Mwalimu Matata achelewe kazini?
    (ii) Kwa nini Mwalimu Matata aliwafundisha wanafunzi uandishi wa insha ya uharibifu wa mazingira?
(e) Waongoze wanafunzi kusimulia habari waliyoisoma kwa maneno machache.
(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **111** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI_KISW.indd 102 7/23/21 3:23 PM

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo.

(b) Wakumbushe wanafunzi alama za uandishi kwa kuuliza maswali.

(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji sahihi kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi sahihi ya alama za uandishi na kusoma kwa hisia.

(d) Waongoze wanafunzi kusoma mmojammoja kwa zamu bila kujali jinsi zao na uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma kadiri muda utakavyoruhusu.

(e) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na uzisahihishe.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo.

(b) Fundisha matumizi ya msamiati ufuatao: *rundika, kinyago, athari, uharibifu, taka, tiririsha, harufu, kansa, ambukiza* na *nusuru.*

(c) Tumia mbinu mbalimbali kama vile maelezo, mjadala, maswali na majibu, igizo au mbinu nyinginezo.

(d) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya neno mojamoja kama lilivyotumika kwenye habari.

(e) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kuzungumza kwa kutumia maneno hayo. Andika sentensi hizo ubaoni na kuangalia kama ziko sahihi. Washirikishe wanafunzi wazisome kwa sauti.

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **111** katika Kitabu cha Mwanafunzi.Wasisitize kuwa sentensi watakazotunga, zisifanane na zile zilizotolewa kwenye mifano.

KIONGOZI_KISW.indd 103 7/23/21 3:23 PM

Somo la 4: Miundo

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu namna ya kutumia miundo katika sentensi.
(b) Nakili ubaoni miundo yote iliyopo zoezi la 3 ukurasa wa **111 - 112** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(c) Waongoze wanafunzi kusoma miundo hiyo ubaoni.
(d) Waongoze wanafunzi kujadili kanuni za miundo hiyo.
(e) Toa mifano ya sentensi zenye miundo iliyopo katika zoezi la 3 ukurasa wa **111 - 112** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(f) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia miundo hiyo kwa mazungumzo na andika sentensi hizo ubaoni.
(g) Angalia usahihi wa sentensi walizozitunga wanafunzi.
(h) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa **111-112** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Sentensi hizo ziwe tofauti na zile zilizotolewa kwenye mifano.

Somo la 5: Mazoezi ya lugha

A. Kuandika sentensi katika wingi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu umoja na wingi.
(ii) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 4 A lililopo ukurasa wa **112** katika Kitabu cha Mwanafunzi kuwaelekeza dhana ya umoja na wingi. Unaweza kuongeza mifano mingine.
(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 A lililopo ukurasa wa **112** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.
(iv) Sahihisha madaftari yao huku ukirekebisha dosari unazozibaini kwa kila mwanafunzi.

Majibu

(i) Wakulima wanapalilia bustani za nyanya.
(ii) Wabunge wametembelea migodi ya wawekezaji.
(iii) Mikono mitupu hailambwi.
(iv) Wanafunzi wanafagia ofisi za walimu wakuu.
(v) Watoto wa shangazi zangu hawapendi viazi.

KIONGOZI_KISW.indd 104 7/23/21 3:23 PM

(vi) Wajasiriamali hufanya kazi kwa bidii.
(vii) Magarimoshi yanasafirisha makontena ya vyakula.
(viii) Wazazi wamewanunulia watoto wao vitabu vipya.
(ix) Wafadhili wamejenga vyoo vya shule kwa gharama nafuu.
(x) Wanafunzi wametunga mashairi ya kisasa.

B. Kuandika KWELI au SI KWELI katika sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kwa kutoa mifano ya sentensi za kujibu KWELI au SI KWELI. Unaweza kutumia sentensi ya kwanza au ya pili kama mfano katika zoezi la 4 B lililopo ukurasa wa **112** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Ongeza sentensi nyingine ili kujenga maarifa katika zoezi hili.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 B lililopo ukurasa wa **112** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) SI KWELI
(ii) KWELI
(iii) KWELI
(iv) SI KWELI
(v) SI KWELI
(vi) SI KWELI
(vii) KWELI
(viii) SI KWELI
(ix) KWELI
(x) SI KWELI

C. Kubadili sentensi kuwa katika kauli taarifa

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya jumla kuhusu namna ya kubadili sentensi kuwa katika kauli taarifa. Waambie wanafunzi kuwa kauli taarifa ni maneno yanayoongewa na msemaji mwingine ambaye ni mtoa taarifa. Mara nyingi, mtoa taarifa hutumia neno … kuwa… au … kwamba… ili kutoa taarifa.

Mfano: **Kauli halisi:** *"Utachaguliwa kujiunga Kidato cha Kwanza," mwalimu alisema.*

Kauli taarifa: *Mwalimu alisema kuwa nitachaguliwa kujiunga Kidato cha Kwanza.*

KIONGOZI_KISW.indd 105 7/23/21 3:23 PM

(ii) Tumia mfano uliopo zoezi la 4 C ukurasa wa **113** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 C lililopo ukurasa wa **113** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Wazazi walisema kwamba simu zao zimevunjika vioo.

(ii) Abiria mmoja alisema kwamba angekuwa safarini siku inayofuata kuelekea Mwanza.

(iii) Mbunge alisema kwamba uchumi wa viwanda huchochea ukuaji wa pato la taifa.

(iv) Mwalimu alituuliza kuwa kwa nini hatuna utamaduni wa kujisomea vitabu.

(v) Mtoto alimwambia mzazi wake kwamba atasoma kwa bidii ili afaulu mitihani yake.

(vi) Abiria aliwaambia askari kuwa dereva aliendesha gari bila uangalifu ndiyo maana walipata ajali.

(vii) Kiranja aliwauliza wanafunzi wenzake kuwa walikuwa wanakimbia kwenda wapi.

(viii) Daktari aliwaambia wananchi kwamba saratani ni ugonjwa hatari sana.

(ix) Mwalimu aliwaeleza wanafunzi kwamba ni bora kuraruka nguo kuliko kuraruka akili.

(x) Muuzaji aliwaambia wanunuzi kuwa redio hizo zilikuwa zinauzwa kwa bei ghali sana.

D. Kuandika sentensi katika wakati ujao

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja nyakati mbalimbali.
Mfano: *wakati ujao, uliopo na uliopita*

(ii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kuzingatia nyakati hizo.

(iii) Wakumbushe kuwa kiambishi kinachoonesha wakati ujao katika kitenzi ni *-ta-*.

KIONGOZI_KISW.indd 106 7/23/21 3:23 PM

(iv) Andika ubaoni sentensi zilizopo ukurasa wa **113** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(v) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi zilizoandikwa ubaoni.

(vi) Waongoze wanafunzi kubadili sentensi kuwa katika wakati ujao. Tumia mifano iliyopo zoezi la 4 D ukurasa wa **113** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(vii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 D lililopo ukurasa wa **113** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Mwanafunzi atakunywa maji safi.

(ii) Shangazi atasafiri kwa basi kuelekea Ruvuma.

(iii) Wawekezaji watajenga hoteli ya kisasa.

(iv) Wanamuziki wataburudisha wananchi kwenye sherehe za uhuru.

(v) Mwalimu atatunga kisamafunzo kizuri sana.

(vi) Wanafunzi wataigiza mbele ya wanafunzi wenzao darasani.

(vii) Wanakijiji watachangia ujenzi wa soko la kijiji.

(viii) Vijana watakwenda kurina asali mwituni.

(ix) Mimi nitatunga mashairi ya kimapokeo na ya kisasa.

(x) Wanajeshi watajenga daraja ili kupitisha vifaa vya kijeshi.

E. Kukanusha sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.

(ii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi na kuzikanusha.

(iii) Waongoze wanafunzi jinsi ya kukanusha sentensi kwa kutumia mfano uliopo zoezi la 4 E lililopo ukurasa wa **114** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano mingine.

(iv) Waongoze wanafunzi kujadili matumizi ya kiambishi cha ukanushi **ha-** kwenye kitenzi.

KIONGOZI_KISW.indd 107 7/23/21 3:23 PM

(v) Ongoza mjadala kuhusu viambishi vya ukanushi. Kumbuka kuwa tunapokanusha vitenzi vilivyo katika wakati uliopo hali ya kuendelea, vitenzi hivyo huishia na irabu **-i**. Pia, kiambishi **-ja-** husimama katika wakati uliopo hali timilifu.

(vi) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 E lililopo ukurasa wa **114** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Shule yetu haijanunua kompyuta mpya.

(ii) Seremala hatatengeneza samani za shule.

(iii) Mafuriko hayajaleta maafa kijijini kwetu.

(iv) Swali hili halijibiki kwa urahisi.

(v) Mjomba hanunui cherehani dukani.

(vi) Wanajeshi hawakulipua ndege ikiwa angani.

(vii) Wakulima hawapati hasara.

(viii) Fundi hajatengeneza gari la shule kwa ustadi mkubwa.

(ix) Mwenyekiti wa Kijiji hakubaliki kwa wanakijiji wenzake.

(x) Babu hajauza mahindi sokoni leo.

F. Kujaza chemshabongo kwa kuzingatia maelezo ya kwenda chini na kwenda kulia

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya somo litakalofundishwa.

(ii) Nakili fumbo na maelekezo ya kwenda chini na kulia ubaoni au kwenye bangokitita kama yalivyo katika zoezi la 4 F lililopo ukurasa wa **114 - 115** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Toa mfano wa kwenda chini swali la kwanza kwa kuuliza swali lifuatalo:

2. Kuwa pekee bila ya mwingine (herufi 5) - PWEKE

(iv) Andika jibu hilo kwenye vyumba vya kuanzia namba 2 kwenda chini. Kila chumba kiandikwe herufi moja tu. Tumia herufi kubwa.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 F lililopo ukurasa wa **114 - 115** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

KIONGOZI_KISW.indd 108 7/23/21 3:23 PM

Majibu

[1]M		[2]P	O	R	I
P		W			
I		[3]E	[4]P	A	
[5]T	A	K	A		
O		[6]E	N	E	[7]A
			D		I
	[8]J	A	A		N
					A

Somo la 6: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo ya somo utakalolifundisha.

(b) Waongoze wanafunzi kujadili kuhusu mada ya utungaji kama ilivyobainishwa katika zoezi la 5 lililopo ukurasa wa **115** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 lililopo ukurasa wa **115** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(d) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, uumbaji wa herufi, matumizi ya herufi kubwa, nafasi kati ya neno na neno, idadi ya maneno, mwandiko mzuri na mtiririko mzuri wa mawazo.

KIONGOZI_KISW.indd 109 7/23/21 3:23 PM

Sura ya Kumi na Nne

Hotuba

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kusikiliza na kusoma hotuba. Pia, atafafanua maudhui yaliyomo kwenye hotuba na kuandika hotuba.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kusikiliza hotuba
(b) kusoma hotuba
(c) kufafanua maudhui yaliyomo katika hotuba
(d) Kuandika hotuba

Mahitaji: vitu halisi, picha (ya kawaida na ya mguso), hotuba za mfano, kalamu rashasha na chati ya maudhui yatokanayo na hotuba

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kufikiri kuhusu mambo ya kuzingatia wakati wa kuandika hotuba katika kipengele cha *fikiri* kilichopo ukurasa wa **116** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Lengo la kipengele cha *fikiri* ni kukuza stadi ya kusikiliza, kuzungumza pamoja na kupata uelewa wa mwanzo alionao mwanafunzi kuhusu somo utakalofundisha.
(b) Waongoze wanafunzi kujadili picha iliyopo ukurasa wa **117** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(c) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari ya **Mkuu wa wilaya ahutubia wanakijiji** iliyopo ukurasa wa **116 - 119** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.
(d) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:
    (i) Mkuu wa Wilaya aliandika nini?
    (ii) Mkuu wa Wilaya aliwahutubia akina nani?
    (iii) Nini maana ya hotuba?
(e) Waongoze wanafunzi kusimulia habari waliyoisoma kwa maneno machache.
(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **119** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI_KISW.indd 110 7/23/21 3:23 PM

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo. Eleza nini unatarajia kifanyike katika somo hili.

(b) Wakumbushe wanafunzi kuhusu alama za uandishi kwa kuuliza maswali.

(c) Soma aya moja kuonesha mfano mzuri wa usomaji kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi ya alama za uandishi na kusoma kwa hisia.

(d) Waongoze wanafunzi kusoma mmojammoja kwa zamu habari ya **Mkuu wa wilaya ahutubia wanakijiji** bila kujali jinsi zao wala uwezo wao. Hakikisha wengi wanapata nafasi ya kusoma.

(e) Baini dosari zinazojitokeza wakati wanafunzi wanasoma na uzirekebishe.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo. Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha msamiati ufuatao: *mwamko, suasua, lengo, hotuba, bashasha, itifaki, hatarini, mkakati, jukumu, chambua, maudhui* na *zindua* kwa kutumia majadiliano, vitu halisi, maelezo, vitendo, picha na maigizo.

(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya neno mojamoja.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa kuzungumza. Andika sentensi hizo ubaoni.

(d) Angalia usahihi wa sentensi walizozitunga wanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **120** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazozitunga, hazifanani na zile zilizotolewa kwenye mifano.

KIONGOZI_KISW.indd 111 7/23/21 3:23 PM

Somo la 4: Methali

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu methali.

(b) Waongoze wanafunzi kutaja methali wanazozifahamu.

(c) Ziandike ubaoni methali hizo.

(d) Waongoze wanafunzi kukamilisha methali kwa kutumia mifano iliyopo zoezi la 3 ukurasa wa **120** katika Kitabu cha Mwanafunzi kama mfano.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa **120** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

1. *hujui kunguni wake*
2. *Kijiti kimoja*
3. *Usiache mbachao*
4. *upate mradi wako*
5. *Usitukane wakunga*
6. *huvutia kwake*
7. *Mficha maradhi*
8. *Mla nawe hafi nawe*
9. *Utajiri ni umande*
10. *na nunduye*

Somo la 5: Mazoezi ya lugha

A. Kutunga sentensi tano (5) zilizo sahihi kutokana na jedwali

Hatua za ufundishaji

(i) Nakili ubaoni jedwali lililopo zoezi la 4 A ukurasa wa **120** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma maneno yaliyopo kwenye jedwali.

(iii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi tano kama mifano.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 A lililopo ukurasa wa **120** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

KIONGOZI_KISW.indd 112 7/23/21 3:23 PM

Majibu

(i) *Anapenda kucheza mpira wa miguu na mpira wa wavu.*

(ii) *Babu ni mfupi lakini mama ni mrefu.*

(iii) *Hakuandika ingawa alikuwa na kalamu.*

(iv) *Tunapenda kusoma kimya na kwa sauti.*

(v) *Kiswahili na Kiingereza ni masomo ya lugha.*

B. Kuandika KWELI au SI KWELI katika sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kwa kutoa mfano wa sentensi za kujibu KWELI au SI KWELI. Unaweza kutumia sentensi ya kwanza au ya pili kama mifano katika zoezi la 4 B lililopo ukurasa wa **121** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Ongeza sentensi nyingine ili kujenga umahiri katika zoezi hili.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 B lililopo ukurasa wa **121** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) *SI KWELI*

(ii) *KWELI*

(iii) *SI KWELI*

(iv) *SI KWELI*

(v) *KWELI*

(vi) *SI KWELI*

(vii) *KWELI*

(viii) *SI KWELI*

(ix) *KWELI*

(x) *KWELI*

KIONGOZI_KISW.indd 113 7/23/21 3:23 PM

C. Kuunda vitenzi kutokana na nomino

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu namna ya kuunda vitenzi kutokana na nomino.

Mfano: ucheshi - cheka

(ii) Waongoze wanafunzi kutaja kitenzi kinachotokana na nomino ucheshi.

(iii) Andika kitenzi hicho ubaoni.

(iv) Nakili ubaoni mifano iliyopo zoezi la 4 C ukurasa wa **121** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 C lililopo ukurasa wa **121** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu

(i) *zuru*
(ii) *dhulumu*
(iii) *chafua*
(iv) *kashifu/kashfu*
(v) *safisha*
(vi) *hutubia/hutubu*
(vii) *iba*
(viii) *tangulia/tanguliza*
(ix) *amrisha/amuru*
(x) *chemsha*

D. Kuzungushia herufi kuunda maneno sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Nakili ubaoni jedwali lililopo zoezi la 4 D ukurasa wa **122** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Toa maelezo ya namna ya kuunda maneno sahihi kutokana na jedwali hilo.

(iii) Toa mfano kwa kuzungushia herufi zinazounda neno la Kiswahili.

KIONGOZI_KISW.indd 114 7/23/21 3:23 PM

(iv) Waongoze wanafunzi kuzungushia herufi zote zinazounda maneno yote sahihi ya Kiswahili yaliyomo kwenye jedwali.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 D lililopo ukurasa wa **122** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

(vi) Buni jedwali linaloshabihiana na lile lililopo kwenye Kitabu cha Mwanafunzi ili kuunda maneno mengine ya Kiswahili.

Majibu

H	O	T	U	B	A	K	R
O	N	I	B	A	K	I	I
M	G	M	I	A	I	S	S
A	E	A	A	D	B	A	A
CH	Z	M	D	H	A	E	S
A	A	U	N	P	I	P	I
M	B	I	L	I	J	U	B
B	U	R	E	K	O	A	O
U	Z	I	O	A	H	W	G
A	D	L	M	J	O	E	A
D	U	A	B	M	A	T	E

Tanbihi: Kubaliana na maneno mengine sahihi yatakayozungushiwa na wanafunzi.

E. Kubadili vitenzi kuwa katika kauli ya kutendeka

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa kuwa mabadiliko yatafanyika katika kitenzi. Kumbuka kauli ya kutendeka inajidhihirisha katika kitenzi kwa kiambishi **-ik-** ,**-ek-** , **-lik-** na **-lek-**.

KIONGOZI_KISW.indd 115 7/23/21 3:23 PM

(ii) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 4 E lililopo kwenye ukurasa wa **122** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 E lililopo ukurasa wa **122** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu

(i) fundishika
(ii) someka
(iii) lipika
(iv) pikika
(v) danganyika
(vi) shoneka
(vii) kubalika
(viii) endesheka
(ix) tosheka
(x) nunulika

Somo la 6: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.

(b) Waongoze wanafunzi kujadili vipengele vya hotuba katika miktadha mbalimbali.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 lililopo ukurasa wa **122** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(d) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, usahihi wa sentensi na mtiririko mzuri wa mawazo.

KIONGOZI_KISW.indd 116 7/23/21 3:23 PM

Sura ya Kumi na Tano

Ufupisho

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atasoma habari na kuifupisha bila kupotosha maana. Pia, atafafanua mafunzo yanayotokana na habari aliyoisoma.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kusoma habari
(b) kubaini mawazo muhimu katika habari
(c) kubaini na kueleza maana ya maneno katika habari
(d) kufupisha habari aliyoisoma bila kupotosha maana

Mahitaji: vitu halisi, michoro, picha (za kawaida na mguso), matini mbalimbali, manila na kalamu rashasha

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kufikiri kuhusu mambo yazingatiwayo wakati wa kufupisha habari katika kipengele cha *fikiri* kilichopo ukurasa wa **123** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(b) Waongoze wanafunzi kujadili picha iliyopo ukurasa wa **125** kwenye Kitabu cha Mwanafunzi.
(c) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari inayohusu Viatu vya Babu iliyopo ukurasa wa **123 - 125** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Wasome bila kufuatisha kwa vidole wala kutoa sauti.
(d) Waulize wanafunzi maswali yafuatayo na wayajibu kwa mazungumzo:
    (i) Kitu gani kimekuvutia katika habari uliyosoma?
    (ii) Umegundua nini zaidi katika habari hiyo?
(e) Waongoze wanafunzi kusimulia habari waliyoisoma kwa maneno machache.
(f) Ongoza mjadala kuhusu funzo linalopatikana kutokana na habari iliyopo ukurasa wa **123 - 125** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(g) Waongoze wanafunzi kujadili kuhusu uhalisia wa habari waliyoisoma katika maisha halisi.
(h) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **126** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI_KISW.indd 117 7/23/21 3:23 PM

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Wakumbushe wanafunzi kanuni na taratibu sahihi za kusoma kwa sauti.

(b) Toa maelezo mafupi kuhusu usomaji sahihi wa habari kwa kuzingatia alama za uandishi.

(c) Waongoze wanafunzi kusoma kwa kasi kwa kuzingatia alama za uandishi.

(d) Waongoze wanafunzi kusoma mmojammoja kwa zamu kwa kuzingatia jinsi zao. Hakikisha wengi wanapata nafasi ya kusoma.

(e) Wakati wanafunzi wanasoma, bainisha dosari zinazojitokeza katika usomaji na uzisahihishe.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri inavyowezekana.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha msamiati ufuatao: *msimu, mbegu, upanzi, ahirisha, kuukuu, mtama, ukarimu, sitisha, staajabu* na *chapuka.*

(b) Unaweza kutumia mbinu mbalimbali, kwa mfano: mbinu ya maelezo, mjadala, igizo au maswali na majibu.

(c) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya neno mojamoja kama lilivyotumika kwenye habari. Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kuzungumza kwa kutumia maneno hayo.

(d) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno yaliyopo ubaoni. Angalia usahihi wa sentensi walizozitunga.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **126** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazozitunga hazifanani na zile walizotunga kama mifano wakati wa kipindi.

KIONGOZI_KISW.indd 118 7/23/21 3:23 PM

Somo la 4: Nahau

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo.
(b) Andika ubaoni nahau utakazofundisha.
(c) Waongoze wanafunzi kusoma kwa sauti nahau zilizopo ubaoni.
(d) Waongoze wanafunzi kueleza maana za nahau zilizopo ubaoni.
Mfano:
(i) cheza shere - fanya mzaha dhidi ya mtu/dhihaki
(ii) weka mtu roho juu - fanya mtu asumbuke
(iii) vaa koti la mtu - tumia cheo cha mtu kwa masilahi binafsi
(iv) inika kichwa - inamisha kichwa kutokana na huzuni au aibu
(e) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia nahau hizo.
(f) Sahihisha makosa yanayojitokeza katika utunzi wa sentensi.
(g) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa **126** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(h) Sentensi watakazotunga zisifanane na zile zilizotungwa darasani kama mifano.

Somo la 5: Misemo

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu maana na dhana ya misemo.
(b) Waongoze wanafunzi kutaja misemo mbalimbali.
(c) Andika misemo hiyo ubaoni.
(d) Waongoze wanafunzi kusoma kwa sauti misemo iliyopo ubaoni.
(e) Waongoze wanafunzi kuibua mjadala kuhusu misemo na kuihusianisha na maisha ya kila siku.
(f) Sahihisha makosa yanayojitokeza.
(g) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa **127** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i)	*e*	*(iv)*	*j*	*(vii)*	*c*	*(x)*	*i*
(ii)	*g*	*(v)*	*k*	*(viii)*	*h*	*(xi)*	*f*
(iii)	*b*	*(vi)*	*d*	*(ix)*	*a*		

KIONGOZI_KISW.indd 119 7/23/21 3:23 PM

Somo la 6: Miundo

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo.

(b) Nakili ubaoni miundo yote iliyopo zoezi la 5 lililopo ukurasa wa **127** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kila muundo.

(d) Waongoze wanafunzi kubaini makosa na kasoro mbalimbali na kuzirekebisha.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 lililopo ukurasa wa **127** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(f) Sentensi zitakazotungwa zisifanane na zile walizotunga darasani. Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

Somo la 7: Mazoezi ya lugha

A. Kupigia mstari neno ambalo ni tofauti na mengine

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo.

(ii) Andika maneno yenye maana sawa ubaoni, kisha weka neno moja lisiloendana na mengine kwa kila kifungu.

(iii) Waongoze wanafunzi kupigia mstari neno lilolo tofauti na mengine.

(iv) Waongoze wanafunzi kujadili majibu yaliyotolewa.

(v) Waongoze wanafunzi kurekebisha makosa yanayojitokeza.

(vi) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 A lililopo ukurasa wa **128** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) rushwa, ufisadi, hongo, huruma

(ii) hadithi, shairi, kisa, simulizi

(iii) baba, shangazi, mama, watoto

KIONGOZI_KISW.indd 120 7/23/21 3:23 PM

(iv) *kicheko, furaha, huzuni, burudani*

(v) *kihusishi, kielezi, kivumishi, utenzi*

(vi) *chui, simba, twiga, ng'ombe*

(vii) *kabati, kitanda, meza, pikipiki*

(viii) *giza, mwanya, upenyo, nafasi*

(ix) *ingawa, cheza, pika, osha*

(x) *jezi, mechi, mchuano, pambano*

B. Kuandika wingi wa sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa.

(ii) Andika sentensi zilizo katika umoja ubaoni, kisha waongoze wanafunzi kuziandika katika wingi.

(iii) Waongoze wanafunzi watunge sentensi mbalimbali katika umoja, kisha wazibadili kuwa katika wingi.

(iv) Waongoze wanafunzi kurekebisha makosa yaliyojitokeza

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 B lililopo ukurasa wa **128** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) *Sisi tumejiunga na vikundi vya uimbaji.*

(ii) *Wanafunzi wamefunga magoli ya vichwa.*

(iii) *Vijana ni mafundi wa nguo za kiume.*

(iv) *Vitabu vimesahaulika jikoni.*

(v) *Njiwa ni ndege wapole.*

(vi) *Mbona hatuwaoni watoto?*

(vii) *Viongozi wanapaswa kuwa mifano ya kuigwa.*

(viii) *Mkiona vinavyong'aa, mjue vimeng'arishwa.*

(ix) *Shangazi zangu wako madukani.*

(x) *Paka wamewakamata panya.*

KIONGOZI_KISW.indd 121 7/23/21 3:23 PM

C. Kuoanisha maneno ya fungu A na fungu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kutoka fungu B katika nafasi iliyoachwa wazi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa.

(ii) Andika ubaoni chati yenye safu mbili za maneno.

(iii) Waongoze wanafunzi kuoanisha maneno hayo kwa kuandika herufi au neno sahihi.

(iv) Waongoze wanafunzi kujadili kuhusu changamoto katika uoanishaji.

(v) Waongoze wanafunzi kurekebisha makosa yaliyojitokeza.

(vi) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 C lililopo ukurasa wa **129** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) *c*
(ii) *e*
(iii) *k*
(iv) *j*
(v) *g*
(vi) *a*
(vii) *i*
(viii) *b*
(ix) *f*
(x) *d*

D. Kutunga sentensi kwa kutumia jedwali

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo.

(ii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia jedwali.

(iii) Waongoze wanafunzi kujadili na kurekebisha kasoro zinazojitokeza.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 D lililopo ukurasa wa **129** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(v) Sahihisha sentensi walizotunga wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi.

KIONGOZI_KISW.indd 122 7/23/21 3:23 PM

E. Kukanusha sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kueleza maana ya ukanushi. Ikumbukwe kuwa ukanushi ni hali ya kukataa maelezo yaliyotolewa katika sentensi. Kwa maana nyingine, ni maelezo hasi kwa yale yaliyotolewa awali.

(ii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi, kisha uziandike ubaoni.

(iii) Waongoze wanafunzi kukanusha sentensi walizotunga.

(iv) Toa maelezo kuhusu mfano uliopo ukurasa wa **129** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 E lililopo ukurasa wa **129 - 130** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Mtima haimbi taarabu.
(ii) Kuku hatembei kwa maringo.
(iii) Sisi sote si watani.
(iv) Leo sijanywa chai kwa vitafunwa.
(v) Kunguru hawakuruka na hawakupaa kama tai.
(vi) Eneo letu halijavamiwa na siafu.
(vii) Mto haujafurika tangu asubuhi.
(viii) Kijana hapendi kuvaa vizuri.
(ix) Nyumbani kwetu hakuna aina mbalimbali za matunda.
(x) Sitanunua gari la thamani kubwa.

F. Kubadili sentensi kuwa katika wakati ujao

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu nyakati, hususani wakati ujao.

(ii) Waongoze wanafunzi kujadili kuhusu wakati ujao.

(iii) Waongoze wanafunzi kueleza mambo ya kuzingatia wakati wa kutunga sentensi katika wakati ujao. Zingatia matumizi ya maneno kama: kesho, keshokutwa na baadaye.

(iv) Waongoze wanafunzi kujadili mfano uliopo kwenye Kitabu cha Mwanafunzi.

(v) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi katika wakati ujao.

KIONGOZI_KISW.indd 123 7/23/21 3:23 PM

(vi) Waongoze wanafunzi kurekebisha makosa yanayojitokeza.
(vii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 F lililopo ukurasa wa **130** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Mama atakunywa uji wa ulezi.
(ii) Dada atachemsha chai ya maziwa.
(iii) Mgonjwa ataruhusiwa kutoka hospitalini.
(iv) Chamando atakula ugali kwa mboga za majani.
(v) Kilimo cha ndizi kitainua kipato cha wananchi.
(vi) Nkindi atachimba viazi vya kuchoma.
(vii) Samaki ataoza kabla ya kupikwa.
(viii) Wanamichezo watarudi nyumbani jioni sana.
(ix) Kima watashambulia shamba la Babu Kigugu.
(x) Njama ya kudhuru mifugo ya Mzee Mombe itagonga mwamba.
(xi) Bomba la jikoni litavuja maji.

Somo la 8: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja mambo ya kuzingatia katika kutunga habari.
(b) Waongoze wanafunzi kutunga habari kuhusu mada yoyote na kuifupisha.
(c) Waongoze wanafunzi kuzingatia alama za uandishi katika utungaji na ufupishaji wa habari.
(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 7 lililopo ukurasa wa **130** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(e) Sahihisha kazi ya mwanafunzi kwa kuzingatia unadhifu wa kazi, mantiki, alama za uandishi, idadi ya maneno ya kwenye habari yasizidi maneno mia mbili (200) na ufupisho uwe kati ya maneno sitini na sabini (60 - 70).

KIONGOZI_KISW.indd 124 7/23/21 3:23 PM

Sura ya Kumi na Sita

Uwasilishaji wa hoja

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kujenga hoja, kueleza hoja katika miktadha mbalimbali na kuwasilisha hoja kwa kuzingatia mpangilio sahihi wa mawazo kimantiki.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kujenga hoja katika miktadha mbalimbali
(b) kueleza hoja katika miktadha mbalimbali
(c) kuwasilisha hoja kwa kuzingatia mpangilio sahihi wa mawazo kimantiki

Mahitaji: chati ya mada za kujengea hoja, chati ya hoja mbalimbali zilizowasilishwa katika mpangilio sahihi, manila, bangokitita na kalamu rashasha

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kufikiri kuhusu mambo ya msingi ya kuzingatia wakati wa ujenzi wa hoja katika kipengele cha *fikiri* kilichopo ukurasa wa **131** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(b) Waongoze wanafunzi kujadili picha iliyopo ukurasa wa **132** kwenye Kitabu cha Mwanafunzi.
(c) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari ya **Mdahalo wa wanyama** iliyopo ukurasa wa **131 - 134** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.
(d) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:
    (i) Uongozi wa Kijiji cha Hewani haukuhamasisha wanyama kufanya nini?
    (ii) Nani alimtangaza Faru kuwa ni mshindi katika uchaguzi?
(e) Waongoze wanafunzi wasimulie kwa maneno machache habari waliyoisoma.
(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **134** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI_KISW.indd 125 7/23/21 3:23 PM

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo.

(b) Wakumbushe wanafunzi kuhusu alama za uandishi kwa kuuliza maswali.

(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji sahihi kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi sahihi ya alama za uandishi na kusoma kwa hisia.

(d) Waongoze wanafunzi kusoma mmojammoja kwa zamu bila kujali jinsi zao na uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma kadiri muda utakavyoruhusu.

(e) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na uzisahihishe.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha matumizi ya msamiati ufuatao: *duni, thabiti, afiki, gombea, kampeni, nadi, wakala, kwamua, thibitisha, teua* na *hema*.

(b) Tumia mbinu mbalimbali, kama maelezo, mjadala, maswali na majibu, igizo au mbinu nyinginezo.

(c) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya neno mojamoja kama lilivyotumika kwenye habari.

(d) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kuzungumza kwa kutumia maneno hayo. Andika sentensi hizo ubaoni na kuangalia kama ziko sahihi. Washirikishe wanafunzi wazisome kwa sauti.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili ukurasa wa **134** katika Kitabu cha Mwanafunzi.Wasisitize kuwa sentensi watakazotunga, zisifanane na zile zilizotolewa kwenye mifano.

KIONGOZI_KISW.indd 126 7/23/21 3:23 PM

Somo la 4: Nahau

Hatua za ufundishaji

(a) Toa mifano ya nahau na uwaongoze wanafunzi kueleza maana za nahau hizo.

(b) Waongoze wanafunzi kutaja nahau mbalimbali wanazozifahamu na kueleza maana zake.

(c) Tumia mfano uliopo zoezi la 3 lililopo ukurasa wa **135** katika Kitabu cha Mwanafunzi kuwaongoza wanafunzi kufanya zoezi la 3 kwenye madaftari yao. Mwanafunzi anaweza kuandika majibu yake kwa herufi tu au maneno au vyote viwili.

Majibu

2. (j) shindwa vibaya
3. (b) laghai, danganya au pumbaza mtu
4. (k) tapeliwa
5. (a) tetea au linda mtu dhidi ya jambo fulani
6. (e) vaa vizuri
7. (h) pongeza au sifia mtu sana
8. (f) konda sana
9. (i) sema waziwazi tabia mbovu ya mtu
10. (g) sema mtu kwa mafumbo
11. (c) fanya starehe

Somo la 5: Miundo

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu namna ya kutumia miundo katika sentensi.

(b) Nakili ubaoni miundo yote iliyopo zoezi la 4 ukurasa wa **135** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kusoma miundo hiyo.

(d) Tumia mifano ya sentensi zenye miundo iliyopo katika zoezi la 4 ukurasa wa **135** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia miundo hiyo kwa kuzungumza na andika sentensi hizo ubaoni.

(f) Angalia usahihi wa sentensi walizozitunga wanafunzi.

(g) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa **135** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Sentensi hizo ziwe tofauti na zile zilizotolewa kwenye mfano.

KIONGOZI_KISW.indd 127 7/23/21 3:23 PM

Somo la 6: Imla

Hatua za ufundishaji

(a) Wakumbushe wanafunzi matumizi ya alama za uandishi, mwandiko mzuri, mpangilio wa aya na nafasi kati ya neno na neno na matumizi ya herufi kubwa.

(b) Soma kwa makini kifungu cha maneno huku wanafunzi wakisikiliza kwa mara ya kwanza.

Siku moja, Sungura aliandaa sherehe ya kuzaliwa kwa mtoto wake. Aliwaalika wageni kadhaa. Wageni walipowasili, Sungura aliwapokea kwa bashasha. Aliwapeleka katika sehemu iliyoandaliwa. Aliwapelekea chakula na vinywaji tele. Wageni wote walifurahia sana sherehe ile. Wageni wote walimzawadia mtoto wa Sungura vitu mbalimbali.

(c) Soma kwa mara ya pili, hatua kwa hatua, huku wanafunzi wakiandika kwenye madaftari yao.

(d) Soma kwa mara ya tatu kifungu chote ili wanafunzi wafanye masahihisho kabla kazi zao hazijasahihishwa.

(e) Kusanya madaftari papo hapo na sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia usahihi wa maneno, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, alama za uandishi, mwandiko mzuri, matumizi ya herufi kubwa na usafi wa kazi.

Somo la 7: Mazoezi ya lugha

A. Kupanga herufi zilizochanganywa ili kuunda neno sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Andika maneno yaliyochanganywa herufi ubaoni.

(ii) Waongoze wanafunzi kupanga herufi ili kupata neno au maneno sahihi.

(iii) Wape nafasi wanafunzi wajaribu kupanga herufi hizo ili kupata maneno kadiri inavyowezekana.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 A lililopo ukurasa wa **136** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) kampeni
(ii) twiga
(iii) mdahalo
(iv) sababu

KIONGOZI_KISW.indd 128 7/23/21 3:23 PM

(v) wasilisha
(vi) sheria
(vii) wakala
(viii) tume
(ix) kijiji
(x) zindua

B. Kupanga sentensi ili zilete mtiririko sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelekezo kuhusu somo utakalofundisha. Kumbuka mtiririko katika habari ni hali ya matukio kuendelea au kufanyika moja kwa moja bila kukatika.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi zilizopo ukurasa wa **136** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waulize wanafunzi kama wamegundua kosa lolote la mtiririko wa mawazo wakati wanasoma sentensi hizo.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 B lililopo ukurasa wa **136** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Siku moja mwalimu wetu alinunua kompyuta.
(ii) Alikuja nayo darasani.
(iii) Aliifungua na kuiunganisha kwenye umeme.
(iv) Alitufundisha namna ya kuitumia.
(v) Aligundua kuwa kuchapa mitihani mwenyewe kunapunguza gharama.
(vi) Aliamua kuchapa mitihani kwa kutumia kompyuta yake.
(vii) Baada ya kuona hivyo, mwanafunzi mmoja aliamua kumwomba baba yake amnunulie kompyuta kwa ajili ya masomo yake.
(viii) Baba yake alikubali na kumnunulia kompyuta mpakato.
(ix) Alitumia kompyuta hiyo kutafuta maarifa na kuchapia kazi zake za nyumbani.
(x) Alijipatia maarifa ya kutosha kwa urahisi.
(xi) Aliwashawishi wanafunzi wenzake kuwaomba wazazi wawanunulie kompyuta ili wazitumie kutafuta maarifa wanapopewa kazi za nyumbani na walimu.
(xii) Wazazi wengi walikubali na kuwanunulia watoto wao kompyuta mpakato.
(xiii) Walihitimu masomo yao wakiwa na ujuzi mkubwa wa kutumia kompyuta.

KIONGOZI_KISW.indd 129 7/23/21 3:23 PM

C. Kuandika neno ambalo ni tofauti na mengine katika safu za maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa.

(ii) Andika maneno yenye maana sawa ubaoni.

(iii) Chopeka neno lenye maana tofauti kwenye kifungu cha maneno. Ongoza wanafunzi kubaini neno hilo.

(iv) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 5 C kuwaongoza wanafunzi kufanya zoezi la 5 C lililopo ukurasa wa **137** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) tajiri
(ii) Sayansi
(iii) ng'ombe
(iv) dawa
(v) ufinyanzi
(vi) papai
(vii) uzururaji
(viii) kikaragosi
(ix) kulima
(x) gulamu

D. Kuandika sentensi katika hali timilifu

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi walizopewa kwa usahihi kwenye vitabu vyao.

(ii) Waulize maswali ili wataje wakati wa kila sentensi wanayoisoma.

(iii) Wanafunzi wanaposoma na kutaja wakati uliotumiwa katika sentensi, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha papo hapo. Kumbuka kuwa viambishi vinavyoonesha nyakati katika kitenzi ni **-na-** (wakati uliopo), **-li-** (wakati uliopita), **-ta-** (wakati ujao), na **-me-** (hali timilifu katika kitenzi).

(iv) Toa maelezo kuhusu hali timilifu.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 D kwa kutumia mifano iliyopo zoezi la 5 D ukurasa wa **137** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Watu wameugua ugonjwa wa malaria kutokana na kuumwa na mbu jike aina ya Anofelesi.

KIONGOZI_KISW.indd 130 7/23/21 3:23 PM

(ii) Mjomba amefanya biashara ya mtandaoni kwa muda mrefu.
(iii) Nimeipenda kalamu yako inavyoandika.
(iv) Rais ametoa msamaha kwa baadhi ya wafungwa nchi nzima.
(v) Tumelima shamba la bibi kwa bidii.
(vi) Watu wameathirika kutokana na mafuriko.
(vii) Babu amesoma kitabu chote cha hadithi.
(viii) Dada amepika maandazi ya kutosha siku ya mwaka mpya.
(ix) Chakula kimepikwa vizuri sana.
(x) Mwanafunzi wangu amekimbia upesi kuelekea nyumbani.

E. Kukanusha sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kufafanua dhana ya ukanushi. Zingatia ukanushi unajidhihirisha katika kitenzi kwa umbo **si** au **ha**.

(ii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi yakinishi. Andika sentensi hizo ubaoni, kisha washirikishe wanafunzi wazikanushe. Andika ubaoni majibu ya wanafunzi, kisha washirikishe kurekebisha makosa kama yapo.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 E lililopo ukurasa wa **137 - 138** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu

(i) Bahati hatatunga hadithi kuhusu wanyama wa porini.
(ii) Mkulima hajavuna karanga kwa wingi shambani.
(iii) Mhitimu hatakunywa soda siku ya mahafali yake baada ya kupokea cheti.
(iv) Baba mkubwa hapendi kula korosho wakati wa jioni.
(v) Mwanafunzi huyu hajaanza utoro hivi karibuni.
(vi) Juma hatakuwa mwandishi mzuri sana wa vitabu vya hadithi za watoto.
(vii) Mama hapendi kusafiri wakati wa usiku.
(viii) Sisi hatutafanya biashara ya kukopesha wakulima zana za kilimo.
(ix) Yeye hachezi darasani wakati wa masomo.
(x) Dada hanunui samaki sokoni.

KIONGOZI_KISW.indd 131 7/23/21 3:23 PM

Somo la 8: Kazi ya kufanya

Hatua za ufundishaji

(a) Andaa mdahalo kuhusu "Kumsomesha mtoto wa kike ni ukombozi kwa jamii nzima" na wape wanafunzi mada hii ili waandae hoja kama ilivyo kwenye zoezi la 6 lililopo ukurasa wa **138** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(b) Ongoza mjadala kuhusu majukumu ya kila kiongozi, kisha waongoze wanafunzi kuchagua viongozi wa mdahalo kama vile mwenyekiti, katibu na mtunza muda.

(c) Mwongoze mfafanua mada jinsi ya kufafanua mada.

(d) Waongoze wanafunzi kuwasilisha hoja kwa kuafiki au kupinga mada katika mpangilio sahihi wa mawazo. Sisitiza ushiriki wa wanafunzi.

(e) Mkumbushe katibu kuandika hoja zinazotolewa na washiriki wa mdahalo.

(f) Mruhusu katibu asome hoja za kila upande na kutangaza mshindi wa mdahalo. Upande utakaopata hoja nyingi, ndio utakuwa mshindi.

(g) Pongeza mshindi na wanafunzi wote walioshiriki katika mdahalo huo.

Somo la 9: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo.

(b) Waongoze wanafunzi kutaja mambo muhimu ya kuzingatia katika ujenzi wa hoja na utungaji.

(c) Waongoze wanafunzi kujadili mambo waliyoyataja kwa usahihi. Rekebisha makosa pale yanapojitokeza.

(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 7 lililopo ukurasa wa **138** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(e) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, herufi kubwa na mtiririko wa hoja.

(f) Baada ya kusahihisha, chagua habari iliyoandikwa vizuri na wanafunzi waisome darasani kwa sauti.

KIONGOZI_KISW.indd 132 7/23/21 3:23 PM